
SportPesa
TZS. 642,668,240
NI YA KWAKO WIKI HII,
BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



**'HOUSEBOI' adaiwa kumnyonga bosi wake hadi kufa kisha kutoweka**

UKURASA 3


ama
ALHAMISI NOVEMBA 4, 2021
AFYA NA MAZINGIRA

ILICHORIPOTI NIPASHE JANUARI... Hatimaye iliyokuwa kliniki chini ya mti kijijini, zahanati rasmi inakuja
Ukurasa 13

SIMULIZI KUTOKA TRAFIKI, TBS, WADAU... Ushindi mkubwa wa ajali barabarani nchini unaoendana na hitaji la mengi
Ukurasa 12

**Kundi la maelfu mabinti, dada zao wakwepeshwa hatari VVU**
•Watafutiwa mbadala wasizurure mtaani

Mabinti wilayani Kahama, wakipata mafunzo ya kiufundi yanayowapa ujuzi wawe mbali na maradhi Ukimwi. PICHA: SHABAN NJIA.

Na Shaban Njia, KAHAMA.

Nipashe
Alhamisi Novemba 4, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580754
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashe

UKURASA 11

# Utapeli mpya waliza maelfu




**KUNDI** latumia jina la MO kudai kutoa mikopo mtandaoni, mwenyewe akanusha... *Endelea uk. 2*

## Sakata machinga lamwibua waziri, atoa majengo NHC

UKURASA 2




Rais mstaafu Jakaya Mrisho Kikwete, akisoma mabango yaliyobebwa na wanafunzi, baada ya maandamano ya kusherehekea miaka 15 ya utoaji wa huduma kwa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu, yaliyoanzia katika viwanja vya Klabu ya Leaders hadi Bwalo la Maofisa wa Polisi Oysterbay, mkoani Dar es Salaam jana. PICHA: MIRAJI MSALA

## Miradi mipya TIC kutoa ajira mpya 130,720

UKURASA 4

MICHEZO **MKWASA: NYOTA WA MECHI YANGA NI REFA** UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6




Mkurugenzi wa Fedha wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), Derick Lugamala (wapili kushoto) na Mkuu wa Biashara na Masoko wa Benki ya Maendeleo, Emmanuel Mwaya (wapili kulia), wakibadilishana mikataba jijini Dar es Salaam jana, baada ya kutiliana saini ya makubaliano ya kutoa mikopo yenye thamani ya Sh. bilioni 2 kwa wakulima. Kushoto ni Meneja wa Usimamizi wa Fedha za wahisani wa Benki ya TADB, Asha Tarimo na Meneja wa Benki ya Maendeleo Tawi la Kariakoo, David Jason. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Utapeli mtandaoni waliza maelfu

**Na Romana Mallya**

UTAPELI mitandaoni umeendelea kuwaliza wananchi baada ya baadhi yao kutumia majina ya watu maarufu na kujitangaza kuwa wanatoa mikopo ya haraka ambayo watu huvutika na wanapotuma fedha, huishia kulia.

Katika mtandao wa Facebook, kuna kundi la watu wanajiita 'Mo Dewji' ambao wananchi wakipiga simu, huwapa maelekezo kuwa watume taarifa zao kwa mtandao wa 'WhatsApp' kwa ajili ya kupata mikopo wanayodai kuitoa ndani ya dakika 15.

Nipashe ilipomtafuta Kisai Salum ambaye ni wakili kwenye kampuni za mfanyabiashara maarufu, Mohammed Dewji 'MO', ili kujiridhisha kama wanawatambua watu hao, alikanusha kuwafahamu. "Nimewasiliana na uongozi wanasema hakuna kitu kama hiki. Hao ni matapeli hatuna MO Foundation inayotoa mikopo, riba na vitu vya namna hiyo. Hakuna kabisa, hatuna huduma za namna hii. "Hatua tunachukua endapo anatokea mtu analalamika kwamba ametapeliwa, anakwenda kufungua kesi polisi kisha hatua za kisheria zinachukuliwa. Hatuna mwakilishi wa MO ambaye anachukua viingilio na kukopesha watu," alisema. Katika mtandao wa Facebook, watu hao wanaojiita 'Mo Dewji' wanawataka wanaohitaji mikopo kutoa kiasi fulani cha fedha kama dhamana kulingana na mkopo husika ili kujiunga.

Watu hao wameainisha viwango vya mikopo na akiba wanavyotoa kuwa kwa wanaotaka mkopo wa Sh. 200,000 wanatakiwa kuweka akiba ya Sh. 22,500 na mkopo utalipwa ndani ya miezi minne. Wanaotaka mkopo wa Sh. 300,000 wanatakiwa kuwa na akiba ya Sh. 35,000 na wataulipa miezi mitano na mkopo wa Sh. 400,000 akiba ni Sh. 40,000 na muda wa marejesho ni miezi sita.

Watu hao wanadai wanatoa mkopo hadi ya Sh. milioni tano na akiba ni Sh. 500,000 na muda wa marejesho ni miaka mitano.

Maelezo mengine wanayotoa ni mhusika kuhakikisha anakuwa na kitambulisho cha mpiga kura au cha NIDA (Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa) pamoja na kiasi cha kutanguliza kwa mkopo anaohitaji na picha yake.

"Ili upate mkopo kwanza unatakiwa uwe na kitambulisho cha mpiga kura au cha taifa na uwe na akiba kulingana na kiasi unachohitaji kuchukua ambacho utaingiza kwetu kama dhamana, utapiga picha kitambulisho chako mbele na nyuma.

"Utapiga picha ukiwa umeshika kitambulisho chako, utatutumia kwenye WhatsApp kwa namba hii (yake) baada ya hapo utaandika maelezo kwa ufupi, wewe ni nani unapatikana wapi, unajishughulisha na nini na unahitaji kiasi gani."

"Baada ya kuandika haya maelezo utatuma namba itakayopokea mkopo, kama ni za benki au simu."

Taarifa yao inamtaka mhusika apige picha akiwa ameshika kitambulisho chake kisha atume namba ya simu itakayopokea mkopo na atakapotuma riba atapokea mkopo wake ndani ya dakika 15. Taarifa pia na imetaja namba ya mhasibu wao ni 0675758461 ambaye ametajwa kwa jina la Ramadhani Kichangamo.

Mwandishi alipopiga namba hiyo na kujitambulisha kama mteja, ndipo Kichangamo alipompa maelekezo ya mkopo kwa kumtaka afuate utaratibu kwa kujiunga WhatsAPP kisha taarifa zingine za namna ya kupata mkopo atazipata huko.

Mwandishi alipotaka kujua zilipo ofisi zao, kijana huyo alitaja jengo la Gymkhana Posta huku akimtahadharisha kuwa kama anashindwa vigezo na masharti vya mtandaoni, aende benki kwa sababu hawataki msongamano ofisini.

Mmoja aliyeingia kwenye mtego wa watu hao ambaye hakutaka jina lake liandikwe gazetini, alisema Jumatatu wiki hii asubuhi alimpigia simu Kichangamo na kumweleza anahitaji mkopo wa Sh. 300,000.

Alisema baada ya maelezo yake ndipo mtu huyo alipomtaka aingie WhatsApp na baada ya kufuata utaratibu wao ikiwa ni pamoja na kupiga picha ndipo akatuma ada ya Sh. 35,000.

"Nilipotuma Sh. 35,000, Kichangamo alinitumia ujumbe mwingine ukithibitisha kupokea akiba yangu na kunijulisha kuwa wanashughulikia akaunti yangu ya marejesho, hivyo alinitaka niingize fedha zingine Sh. 17,000 kwa ajili ya kufungua akaunti hiyo. "Ujumbe huo ulieleza kuwa baada ya kufunguliwa akaunti, watakapoweka mkopo watajumulisha fedha za kufungua akaunti, na watajumlisha na fedha ya kutolea mkopo, hivyo jumla itakuwa Sh. 325,000. Pia waliniambia marejesho yangu kwa mwezi ni Sh. 60,000 kwa muda wa miezi mitano," alisema.

Alisema baada ya maelezo hayo, alipomweleza kuwa hataweza kutuma fedha nyingine, Kichangamo alimjulisha kuwa fedha zake zitarudi ingawa mpaka sasa hajapokea chochote.

Gazeti hili lilipomtafuta Kaimu Kamanda wa Mkoa wa Kipolisi wa Ilala, Kamishna Msadizi (ACP) Moses Fundi, alisema hawajapokea malalamiko yoyote ya wananchi kuhusiana na utapeli unaofanywa na watu hao.

"Ushauri wetu kwa wananchi wakitaka mikopo waende kwenye taasisi za fedha ambazo zinatambuliwa kisheria na si kutaka mikopo ya mitandaoni ambayo mwisho wa siku wanajikuta wanaibiwa fedha zao,"

**UNHCR**
United Nations High Commissioner for Refugees
Haut Commissariat des Nations Unies pour les réfugiés

**TENDER NOTICE**

**REQUEST FOR PROPOSAL: No. RFP/2021/KAS/SUP/001**

**FOR THE CONSTRUCTION OF CLASSROOMS AND LATRINES FOR HOST COMMUNITY IN KAKONKO, KIBONDO AND KASULU**

1. **Background:**
The Office of the United Nations High Commissioner for Refugees (UNHCR), Representation Office in Dar es Salaam invites capable, qualified and eligible Firms/Contractors duly registered with the Tanzanian Government, and by Contractors Registration Board (CRB) to make firm offers to carry out the work as per the scope of works, specifications and Terms of Reference for construction of UNHCR office in Kigoma.

2. **Eligibility:**
Contractors duly registered with relevant government authorities, with sound financial basis, relevant experience, reputed clientele and with knowledge of how to meet UNHCR's requirements are invited to participate in the bidding process.

Kindly download the tender documents in the below link:

https://drive.google.com/drive/folders/1RlhoxKP-xXoHNKguM0GwAP6MZ5roddFV?usp=sharing

If you fail to access the link, please write to kyoma@unhcr.org copy kioko@unhcr.org, ishobeza@unhcr.org and jacksonw@unhcr.og

| | |
|---|---|
| Deadline for receiving requests for clarification | Tuesday 23rd November 2021 at 2359hrs EAT |
| Site Visit | 16th & 17th November 2021 at Kakonko/Kibondo from 1000hrs EAT |
| Site Visit | 18th & 19th November 2021 at Kasulu from 1000hrs EAT |
| Deadline for submission of offers | Tuesday 30th November 2021 at 1600hrs EAT |

**CRUCIAL DATES FOR THIS REQUEST FOR PROPOSAL**

216553402

## Sakata machinga lamwibua Waziri, atoa majengo NHC

**Na Munir Shemweta**

MAJENGO matatu ya Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) katika mitaa ya Mkunguni na Nyamwezi, Kariakoo jijini Dar es Salaam, yameainishwa kutumiwa na wafanyabiashara wadogo, maarufu kama machinga.

Kuainishwa kwa majengo kumetokana na ziara ya Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk.Angeline Mabula, juzi, hivyo kuagiza NHC kuyaboresha kulingana na mahitaji ya wafanyabiashara hao.

Dk. Mabula alifanya ziara hiyo kwa lengo la kuangalia namna bora ya kuwawezesha wafanyabiashara hao wadogo, kutumia majengo ya shirika hilo kufanyia biashara.

Hatua ya Naibu Waziri ilitokana na wafanyabiashara hao kuandika barua Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kupatiwa sehemu za kufanyia biashara kwenye majengo ya NHC yaliyoko Kariakoo baada ya serikali kuamua kuwaondoa maeneo ya barabarani, waliyokuwa wakifanyia shughuli zao.

Ombi la wafanyabiashara hao lilisababisha TAMISEMI kuiomba Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kuangalia namna ya kuwasaidia kuwapatia sehemu kwenye baadhi ya majengo ya NHC, shirika ambalo liko chini ya Wizara ya Ardhi.

Hatua hiyo ya TAMISEMI ilimfanya Naibu Waziri Mabula kufanya ziara ya kukagua majengo ya NHC yaliyoainishwa kwenye mitaa ya Tandamti na Msimbazi kwa ajili ya kujiridhisha na kuona kama majengo hayo yanaweza kufaa kwa biashara za machinga.

Hata hivyo, majengo ya NHC yaliyoainisha katika mitaa ya Msimbazi na Nyamwezi, yameonekna kutokidhi vigezo lakini Naibu Waziri na timu ya viongozi wa NHC walibaini majengo mengine matatu yatakayofaa kwa shughuli za machinga.

Akiwa ameambatana na Kaimu Mkurugenzi wa Uwekezaji na Uendelezaji Biashara wa Shirika la Nyumba la Taifa, William Genya, Kamishna wa Ardhi Msaidzi Mkoa wa Dar es Salaam, Idrisa Kayera, na Meneja wa NHC Mkoa wa Ilala, Erasto Chilambo, juzi, Dk. Mabula alitembelea majengo kadhaa na kuridhika majengo matatu yaliyoko mitaa ya Mkunguni na Nyamwezi kwa kueleza kuwa majengo hayo yanaweza kuboreshwa na kutumika.

Akielezea uamuzi wa kufanya ziara hiyo, Naibu Waziri alisema unalenga kuangalia namna bora ya kuwasaidia wafanyabiashara wadogo hasa baada ya TAMISEMI kupeleka ombi na kubainisha kuwa msisitizo ni kuwapatia machinga maeneo ya kudumu yakiwa na miundombinu.

"TAMISEMI waliainisha mitaa ya Tandamiti na Msimbazi kwa ajili ya wafanyabiashara wadogo, lakini maeneo hayo yameonyesha kutokidhi mahitaji. Lakini tumeona majengo matatu yaliyoko mitaa ya Nyamwezi na Mkunguni, karibu kabisa na Soko Kuu la Kariakoo, yanaweza kufanyiwa mabadiliko kwa ajili ya shughuli za kuhudumia mahitaji ya machinga," alisema.

Hata hivyo, Dk. Mabula aliitaka NHC kulichukulia suala hilo kwa umuhimu mkubwa na haraka kutokana na changamoto zake na kusisitiza kuwa wakati hatua za utekelezaji maendelezo ya majengo yaliyoainishwa ukifanyika, ni vyema kila kitu kikawekwa ili wafanyabiashara wakaelewa mwelekeo wao.

"Hili ni suala la msingi na lazima lifanyike kwa haraka na sisi wizarani tulipate taarifa mapema na tujue majengo haya yatachukua watu wangapi na uendelezaji wake utachukua muda gani ili wafanyabiashara wajue kuna eneo maalum la kufanya biashara kama ambavyo wamekusudia wao kupatiwa," alisema.

HABARI KITAIFA

# ‘Houseboi’ adaiwa kumnyonga kwa kamba bosi wake hadi kufa

**Na Christina Mwakangale**

KIJANA wa kazi za nyumbani ‘house boy’ (jina tunalihifadhi), anadaiwa kumuua bosi wake kwa kumnyonga kwa kamba ya katani kisha kutokomea.

Tukio hilo lilitokea Jumatatu, Bombani Kata ya Pugu, jijini Dar es Salaam.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Ilala, Kamishna Msaidizi wa Polisi Moses Fundi, aliiambia Nipashe jana kwamba mtuhumiwa huyo alimnyonga Cecilia Songomba (56), ambaye alikuwa mkunga mstaafu.

“Inasemekana mtuhumiwa ni mkazi wa Kaliua, mkoani Tabora, walikuwa (familia ya marehemu( wamekaa naye kwa wiki mbili, hiyo nyumba walikuwa wanakaa watu watatu tu, mama (Cecilia), baba ambaye ni mume na huyo kijana,” alisema Kamanda Fundi.

Alisema mume wa Cecilia ambaye wakati wa tukio alikuwa mjini, aliporejea nyumbani aligonga mlango bila kufunguliwa ndipo alipoamua kuruka ukuta ili aingie ndani.

“Alipoona anagonga mlango hafunguliwi, akaona aruke ukuta, aliporuka akakuta huyo mama amenyongwa kwa kufungwa chooni, kwa kamba ya katani.

Kamanda Fundi alisema mtuhumiwa hajakamatwa kwa kuwa baada ya tukio hilo alitoroka.

# AfCHPR yalia hukumu zake kutotekelezwa

**Na Romana Mallya**

RAIS mstaafu, Jakaya Kikwete, ameungana na Rais wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu, Jaji Imani Aboud, kusherehekea miaka 15 tangu kuanzishwa kwa mahakama hiyo, ambayo inakabiliwa na tatizo kubwa la nchi wanachama kutotekeleza uamuzi wanaoutoa.

Katika sherehe hizo, Kikwete aliungana na viongozi wa mahakama hiyo na wadau wengine katika matembezi yaliyofanyika kuanzia viwanja vya Leaders, Upanga hadi Polisi Officers Mess, Oysterbay.

Baada ya matembezi hayo, Jaji Imani alisema kwa asilimia zaidi ya 75 ya hukumu ambazo wamezitoa katika mahakama hiyo hazijatekelezwa na nchi mwanachama.

“Matatizo makubwa yamekuwa ni uamuzi wa mahakama hautekelezwi na nchi husika mpaka sasa ni asilimia saba tu ya uamuzi wetu tuliotoa ndiyo umeweza kutekelezwa na asilimia 18 umetekelezwa kwa kiasi.

“Asilimia zaidi ya 75 hayajatekelezwa, hili ni tatizo kubwa kwa sababu tunataka tusikilize mashauri, tutoe hukumu na tuone yanatekelezwa kwa yule ambaye amekuja na kudai haki amepata haki yake.”

Rais huyo alisema ndiyo maana katika kusherehekea miaka 15, wamekuwa na mazungumzo na wale waliyoianzisha mahakama kutoka mataifa mbalimbali ya Afrika ambayo ni 55.

“Tumeona tuzungumze kwa nini uamuzi unaotolewa na mahakama hii hautekelezwi, kuna matatizo gani? Kama yapo namna gani tunatatua na kutafuta suluhu ya kuyaondoa kwa sababu wanapokuwa hawatekelezi, tunakuwa hatujui lakini kwa mikutano hii kuanzia juzi (Jumatatu) tumekuwa tukizungumza na wawakilishi wengi wamekuwa wazi,” alisema.

Alisema wamekuwa na shughuli mbalimbali pamoja na mikutano miwili mikubwa ya kimataifa ambayo ilimalizika jana ambayo imejadili matatizo na namna gani kumekuwa na tatizo la utekelezaji wa uamuzi wa mahakama hiyo.

“Tangu tumeanza kazi, mahakama imeweza kusikiliza kesi zaidi ya 150 na kwa ujumla tunakesi 300 katika mahakama yetu, uamuzi tunaotoa tunaamini ni uamuzi wa haki dhidi ya nchi.

“Mashauri mengi yanayoletwa ni kulalamika labda nchi husika imevunja haki za binadamu ama ya mtu mmoja au kikundi cha watu.”

Jaji Imani alisema katika utoaji haki lazima wahakikisha uamuzi unaotolewa na mahakama unatekelezwa.

“Tunategemea pia kufanya mkutano pamoja na mabalozi wa nchi zote 55 mwezi ujao ili kutafuta njia bora ya kuboresha kazi za mahakama,” alisema.

Kuhusu mafanikio, Jaji Imani alisema wanaendelea kuitangaza mahakama hiyo kwa sababu inawezekana siyo Waafrika wote wanaijua ipo kwa ajili yao.

“Kwa sasa watu wanaelewa, mfano Tanzania tuna kesi zaidi ya asilimia 80 katika mahakama, tumekuwa na ufahamu zaidi, asilimia 80 ya kesi zinatoka Tanzania ujue kwamba mataifa mengine hawajui, tumekuwa tukitembelea taifa moja baada ya lingine kukuza uelewa wa mahakama,” alisema.

Pia alisema wameweza kutoa ripoti mbalimbali, vitabu vya kujifunza ambavyo wanaamini mahakama za ndani ya nchi wanaweza kutumia uamuzi wa mahakama ya Afrika kufanya uamuzi wao kama nyenzo inayowapa mwelekeo wa masuala mbalimbali.

Hata hivyo, Rais huyo alisema kwa sababu mahakama hiyo ni ya nchi za Afrika ndizo zitakazoamua namna gani utendaji wao wa kazi wa majaji na watumishi katika kuiboresha zaidi na kuondoa matatizo na kuongeza ubora wa kazi.

Rais mstaafu Kikwete alisema wakati akiwa Waziri wa Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Rais wa awamu ya tatu, Benjamin Mkapa, aliamua kusaini mkataba wa itifaki wa kuanzishwa kwa mahakama na kuomba Tanzania iwe mwenyeji wake.

“Ninashukuru mahakama hii imekaa miaka 15 na sasa inasherehekea miaka 15. Wamekuja Dar es Salaam kufanya mkutano na kumbukumbu ya mahakama hii, tunawapongeza kwa hatua waliyofikia,” alisema.


EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

**OMBI LA KUONESHA NIA KWA AJILI YA UTOAJI WA HUDUMA YA SAMANI ZA OFISI PAMOJA NA UWEKAJI WA SAMANI KATIKA OFISI**
**KUMBUKUMBU 0010007217**

Kampuni ya Kimataifa ya Mafuta na Gesi ya TotalEnergies East Africa Midstream B.V. inaalika taasisi zenye weledi na uzoefu kuonesha nia ya kutoa huduma ya uwekezaji wa vyombo vya ofisini.

Mradi wa EACOP unahusisha ujenzi na uendeshaji wa bomba litakalofukiwa chini ya ardhi litakalovuka mipaka ya nchi mbili na litakalosafirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Pwani ya Mashariki ya Tanzania kwa ajili ya kusafirisha mafuta hayo kwenda katika masoko ya Kimataifa. Bomba hili litaanzia Kabaale katika wilaya ya Hoima nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoani Tanga nchini Tanzania. Urefu wa Bomba ni kilomita 1,443, kati ya hizo, kilomita 1,147 zitakuwa Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI KUHUSU MAWANDA YA HUDUMA:**

- EACOP inahitaji huduma kutoka kwa mtoa huduma mwenye uzoefu na sifa nzuri ya kutoa huduma za samani za ofisi pamoja na kuziweka katika ofisi ipasavyo.
- Madawati na meza za kufanyia kazi (vituo vya kazi vinavyoweza kuongezwa na kupunguzwa urefu wakati wa matumizi).
- Meza na viti vya vyumba vya mikutano (kiwango cha kawaida na kiwango cha vyumba vya mikutano).
- Viti vya ofisini vinavyoweza kurefushwa au kufupishwa na vilivyo undwa kwa ajili ya kutoa usaidizi bora kwa mgongo wakati wa kukaa (ergonomic).
- Makabati ya kuhifadhi mafaili (Credenzes).
- Kabati za kuhifadhi vitu mbali mbali.

**VIGEZO MUHIMU:**

Taasisi zitakazoonesha nia zinaalikwa kuambatanisha maombi yao pamoja na taarifa zifuatazo:

- Uthibitisho wa Uzoefu, utendaji, na uwezo katika kutekeleza kazi zilizoainishwa katika mawanda ya kazi, kwa viwango vya juu nchini Tanzania, kwa kufuata viwango vya kitaifa na kimataifa (ikiwa ni pamoja na Viwango vya Shirika la Fedha la Kimataifa (IFC), na uzoefu wa angalau miaka 5 katika utendaji wa huduma kama hizo ndani ya Tanzania au Kimataifa.
- Uthibitisho wa watendakazi husika wenye vigezo na uzoefu katika uwekaji wa samani katika ofisi.
- Inashauriwa, mwonyesha nia atume maombi ya kusajiliwa na kanzi data ya EWURA (LSSP) kama mtoaji namsambazaji wa huduma ndani ya nchi wakati wa kuwasilisha ombi la kuonesha nia ya kutekeleza shughuli za progamu.
- Kuzingatia Kanuni za maudhui ya Ndani za mwaka 2017 pamoja na tafsiri ya Kampuni ya Ndani.
- Uwezo wa kifedha kuweza kutoa huduma zinazohitajika ikiwa ni pamoja na kuwasilisha mahesabu ya fedha ya mwaka 2017.

- Uthibitisho wa sera ya ndani ya Afya, Mazingira na Usalama, taratibu na mchakato kulingana na viwango vya ndani vya viwanda vya kazi husika.
- Uthibitisho wa usajili katika mamlaka husika ndani ya nchi kwa ajili ya utoaji wa huduma husika.
- Uthibitisho wa usajili wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) pamoja na cheti cha uthibitisho wa kulipa kodi kwa mwaka wa fedha uliopita.

Taasisi zenye nia ya kuleta maombi na ambazo zina uwezo na rasilimali za kutekeleza shughuli au kazi zilizoorodheshwa hapo juu zinapaswa kueleza nia yao kwa lugha ya kiingereza pamoja na kuambatanisha nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe kwa **eacoptz.eoi.1000001@totalenergies.com** (ukubwa wa barua pepe 20 Mb) saa au kabla ya saa **11 jinni** za Afrika Mashariki (EAT) tarehe **....Novemba 2021.** Kichwa cha Habari cha barua pepe kiwe ni kumbukumbu namba husika tu. Kichwa cha Barua Pepe kiwe ni **0010007217.**

**Muhimu:** Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na taasisi zitakazoonyesha nia iii kutengeneza orodha ya taasisi za awali zenye vigezo vinavyotakiwa. Taasisi zitakazokidhi vigezo iu ndiyo zitapokea na kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA) pamoja na mwaliko wa kuwasilisha zabuni katika kuendeleza mchakato wa zabuni. Maelezo yote ya kuonyesha nia yanapaswa kuandikwa kwa lugha ya Kiingereza.

216552602

## Sabaya augua, kesi yakwama

**Na Allan Isack,** ARUSHA

KESI ya Uhujumu Uchumi inayomkabili aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya (34) na wenzake sita, jana ilishindwa kuendelea kusikilizwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi, Mkoa wa Arusha, baada ya Wakili wa mashtakiwa wa kwanza, Mosses Mahuna, kuomba kuahirisha kesi hiyo kwa kuwa mteja wake ni mgonjwa.

Mahuna na Faudhia Mustapher, wanaomtetea Sabaya, waliomba ahirisho hilo mbele ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha, Patricia Kisinda.

Pamoja na taarifa za ugonjwa wa mteja wao kuzipata ndani ya muda mfupi, lakini ilitakiwa kuomba ahirisho hilo, kukubaliwa na mahakama kwa kuwa kesi hiyo ilitakiwa kuendelea kusikilizwa mahakamani huko jana.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Oftem Mtenga, alikubaliana na hoja ya ahirisho la kesi hiyo na aliiomba mahakama wakati ujao mawakili wa utetezi kuwasilisha cheti cha daktari mbele ya mahakama ili kuthibitisha kwamba mteja wao ni mgonjwa.

Mtenga, alisema upande wa Jamhuri unapaenda kuimaliza kesi hiyo kwa haraka bila ya ucheleweshaji, lakini kwa hali ilivyokuwa ya kuahirisha kesi kwa sababu ya ugonjwa na bila kuwasilisha cheti cha daktari ni ukiukwaji mkubwa wa sheria.

Kauli hiyo ilimwibua Mahuna na kuwasilisha cheti cha daktari kilichoonyesha Sabaya, alipata huduma ya matibabu katika Hospitali ya Magereza na alitakiwa kupata mapumziko na cheti kiliwasilishwa na askari Magereza.

"Mheshimiwa Hakimu kwa sababu Jamhuri wamesema kuwa wanaitaka kesi hii kuisha mapema na kusiwepo na ucheleweshaji sasa tunaomba tuendelee na kesi kwani mteja wetu ameridhia hilo," alida Mahuna.

Baada ya majibishano hayo, Hakimu Kisinda alisema anaungana na hoja ya awali ya Wakili Mahuna ya kuahirisha kesi hiyo, hadi Novemba 4 (leo) na kuwataka waendesha mashtaka wa serikali kuhakikisha wanakwenda na shahidi ili kesi hiyo iendelee.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Felix Kwetuki, alimweleza hakimu kuwa shahidi namba saba katika kesi hiyo, ambaye ushahidi wake ulisitishwa ataendelea kutoa ushahidi na tayari alikuwa mahakamani.




Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Uwekezaji, Geoffrey Mwambe, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dodoma jana, katika mwendelezo wa mawaziri kutoa taarifa zao za mafanikio ya serikali, kuelekea maadhimisho ya Miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania Bara ambapo kilele chake itakuwa Desemba 9, mwaka huu. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Miradi mikubwa ya kimkakati kuzalisha ajira mpya 130,000

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KITUO cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kimesajili jumla ya miradi mikubwa ya kimkakati kwa kupewa hadhi ya miradi mahiri ipatayo 43, ambayo itatoa ajira 130,720.

Sambamba na kutoa ajira hizo kwa Watanzania, pia miradi hiyo inatarajia kuwekeza kiasi cha Dola za Marekani milioni 12,278.00

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Geofrey Mwambe, alibainisha hayo jana alipokuwa akitoa taarifa ya mafanikio ya wizara hiyo katika miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania Bara.

Alisema miradi hiyo inahusisha sekta mbalimbali, ambazo ni kilimo, uzalishaji viwandani, majengo ya biashara, ujenzi na madini.

Alisema baadhi ya miradi iliyofanikishwa kupata hadhi ya uwekezaji kupitia NISC ni wa Mount Meru Millers, Mlimani City, Dangote Industries Limited na Mtibwa Sugar Estates Ltd.

Mingine ni Kagera Sugar Estate, Kilombero Sugar Company, Kilombero Plantations Limited (KPL), Tanga Cement Company Limited, TANCOAL Energy Limited na Goodwil Ceramics (Tz) Limited.

"Tangu serikali ilipoanza kutekeleza Sera ya Taifa ya Uwekezaji na Sheria ya Uwekezaji Tanzania, wastani wa uwekezaji unaopimwa kwa kuangalia uwiano wa uwekezaji yaani ukuzaji Rasilimali kwa Pato la Taifa umekuwa ukiongezeka," alisema Mwambe.

Vilevile, alisema takwimu zinaonyesha uwiano wa ukuzaji rasilimali kwa Pato la Taifa umekua kutoka asilimia 14.7 mwaka 1997 hadi asilimia 39.7 mwaka 2019.

"Hivi ni viwango vikubwa ukilinganisha na wastani wa nchi za Afrika wa asilimia 21 hadi asilimia 22 na nchi zilizoendelea wa asilimia 23 hadi 25," alisema.

Aidha, alisema uwekezaji wa mitaji kutoka nje umeongezeka kutoka Dola za Marekani bilioni 0.73 mwaka 1996 hadi Dola za Marekani bilioni 2.18 mwaka 2013 na hadi Dola za Marekani bilioni 1.01 mwaka 2020. Alisema serikali imefanikiwa kuanzisha kituo cha utoaji huduma za uwekezaji mahali pamoja kwa kuleta pamoja wizara na taasisi 12 ambazo ni Wizara ya Kazi (masuala ya vibali vya kazi), Wizara ya Ardhi (masuala ya Ardhi-Derivative rights), Idara ya Uhamiaji (Masuala ya vibali vya ukaazi, TIC (kuratibu na kutoa cheti cha vivutio), BRELA (Usajiri wa Kampuni), NIDA, TBS, NEMC na OSHA.

Pia, alisema serikali imeendelea kuratibu na kufanya utafiti na tathmini za mazingira ya biashara, uwekezaji na uchumi ambazo hutumika kuwezesha maamuzi katika mikutano ya majadiliano kati ya sekta ya umma na sekta binafsi.

"Serikali imeratibu na kufanya utafiti kuhusu bidhaa za mbao zilizohandisiwa, fursa zake na kuandaa mapendekezo ya maboresho yanayohitajika ili kuchochea uwekezaji katika sekta ya misitu," alisema.

Kadhalika, alisema serikali imeratibu na kuandaa andiko kuhusu changamoto za MSMEs kwa sekta ndogo ya misitu ya kibiashara na bidhaa za misitu.

# Shahidi kesi ya Mbowe augua ghafla

**Na Kulwa Mzee**

SHAHIDI wa sita aliyetarajiwa kupanda kizimbani jana kutoa ushahidi katika kesi ya ugaidi imayomkabili Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe na wenzake watatu ameugua ghafla na kushindwa kufika mahakamani.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Robert Kidando, alidai hayo jana Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi mbele ya Jaji Joackim Tiganga, wakati kesi hiyo ilipotakiwa kuendelea kusikilizwa.

"Mheshimiwa Jaji kesi ilikuja kwa ajili ya kuendelea na shahidi wa sita kama tulivyopanga, jana (juzi) tulimwandaa afike kutoa ushahidi, lakini amepatwa tatizo la kiafya akashindwa kufika asubuhi hii mahakamani.

"Tunaomba ahirisho ili tupate shahidi mwingine tuendelee siku ya kesho," alidai Kidando.

Akijibu, Wakili Peter Kibatala alidai kwa upande wao walijiandaa, lakini kama hali iko hivyo hawana la kufanya na kusisitiza wajitahidi kupata shahidi mwingine ili kesi iendelee.

Jaji Tiganga alisema kutokana na maombi ya upande wa Jamhuri kuomba kuahirisha kwa sababu shahidi aliyepangwa kapata maradhi ya kushindwa kufika mahakamani, aliahirisha shauri hilo.

"Shauri hili linaahirishwa hadi kesho (leo) andaeni shahidi au mashahidi kwa ajili ya kesi kuendelea," alisema Jaji Tiganga.

Shahidi wa tano alitoka Kampuni ya MIC Tanzania Limited, maarufu Tigo, Fredy Kapara, ambaye alidai alipewa namba ya kuchunguza ilikuwa 0719 933386 ya Freeman Mbowe, ilituma Sh. 500,000 kwenda kwa Luteni Dennis Urio namba 0787 555200 ambayo ilionekana kwenye usajili.

Shahidi alidai Julai 2021 alipokea barua kutoka kwa Kamishna wa Upelelezi wa Kisayansi akitaka taarifa za mteja mwenye namba 0719 933386 aliomba miamala kuanzia Juni mosi mwaka 2020 hadi Julai 31, mwaka 2020.

Alidai alivyoingiza namba hiyo katika mfumo alipata taarifa hizo akaziprinti na kuziwasilisha zilipohitajika.

Aliomba kutoa kama kielelezo barua aliyoombwa kuchunguza namba, barua aliyoandika baada ya uchunguzi, taarifa za miamala ya fedha na taarifa za usajili.

Upande wa Jamhuri haukuwa na pingamizi kwa vielelezo hivyo kupokelewa, Mahakama ilipokea na kuvipa P6, P7, P8 na P9.

Akisoma vielelezo hivyo alidai namba 0719 933386 ilituma fedha Sh. 500,000 akiwa maeneo ya Mikocheni wilayani Kinondoni kwenda kwenye namba 0787 555200 ambayo hakutaja jina kwa madai taarifa za namba hiyo zinapatikana Airtel.

Namba hiyo iliyotumiwa fedha katika kuangalia kwenye usajili inasoma jina la Dennis Urio ambaye anatajwa katika kesi hiyo ya ugaidi kuwa miongoni mwa shahidi.

Luteni mstaafu Dennis Urio katika maelezo ya ushahidi yaliyopo mahakamani inadaiwa alipewa kazi na Mbowe ya kumtafutia makomandoo waliofukuzwa kazi jeshi au waliostaafu ili afanye nao kazi.

Alidai namba 0719 933386 alipoichunguza usajili alibaini ilisajiliwa awali mwaka 2016 na ikasajiliwa kwa mara ya pili kwa alama ya vidole Julai 16, 2019.

Pia, alidai baada ya kukamilisha uchunguzi aliitwa Julai 8, mwaka huu Kituo cha Polisi cha Kati kwa ajili ya kutoa maelezo na alikwenda.

Washtakiwa katika kesi hiyo ni Mbowe, Adamu Kasekwa, Mohammed Ling'wenya na Halfani Bwire ambao wanakabiliwa na mashtaka sita ikiwamo kula njama kufanya vitendo vya kigaidi kati ya Mei mosi na Agosti 5, mwaka 2020 katika mikoa ya Morogoro, Moshi, Arusha, Dar es Salaam, Mbeya na Mwanza.

# MATANGAZO

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

## IMEDURIWA - OMBI LA KUONESHA NIA YA KUTOA HUDUMA ZA UCHAPISHAJI TAARIFA PAMOJA NA BIDHAA ZENYE CHAPA KATIKA MRADI WA BOMBA LA MAFUTA GHAFI LA AFRIKA MASHARIKI. KUMBUKUMBU. 0010007126

Kampuni ya Kimataifa ya Mafuta na Gesi ya TotalEnergies East Africa Midstream B.V, inaalika taasisi na kampuni zenye weledi na uzoefu katika Nyanja ya uchapishaji wa nyaraka za mawasiliano katika mifumo mbalimbali pamoja na kutoa huduma ya bidhaa zenye chapa (Large Scale Printing and Products Branding) katika Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP).

Mradi wa EACOP unahusisha ujenzi na uendeshaji wa bomba litakalofukiwa chini ya ardhi litakalovuka mipaka ya nchi mbili na litakalosafirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Pwani ya Mashariki ya Tanzania kwa ajili ya kusafirisha mafuta hayo kwenda katika masoko ya Kimataifa. Bomba hili litaanzia Kabaale katika wilaya ya Hoima nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoani Tanga nchini Tanzania. Urefu wa Bomba ni kilomita 1,443, kati ya hizo, kilomita 1,147 zitakuwa Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI KUHUSU MAWANDA YA HUDUMA**

KAMPUNI inahitaji huduma za kampuni ya mawasiliano kutoa usaidizi katika moja au huduma mbalimbali tajwa kulingana na mahitaji:

- Huduma ya uchapishaji taarifa za mawasiliano katika mifumo mbalimbali.
- Kutoa huduma ya bidhaa zenye chapa ikiwa ni pamoja na mbao za matangazo na masanduku ya maoni yenye chapa.

**VIGEZO MUHHIMU**

Makampuni au mashirika yatakayoonesha nia, yanaalikwa kutuma maombi pamoja na nyaraka zifuatazo:

- Uthibitisho wa uzoefu wa utendaji kazi bora pamoja na sampuli za kutekeleza kazi za usaidizi katika mawanda ya mawasiliano ya nia husika, kampuni au Taasisi inaweza kuonyesha nia kwa zabuni moja au zaidi kati ya zilizoorodheshwa hapo juu. Katika hatua hii, sampuli zote za kazi za mawasiliano zinatakiwa kuwasilishwa kupitia uzi wa taarifa (link) ambao hautarajii kuisha muda wake.
- Uthibitisho wa uwezo mfano kuwa na vifaa, miundo mbinu pamoja na muundo wa timu ya watendaji.
- Uthibitisho wa kufanya kazi katika miradi mikubwa yenye uhitaji mkubwa wa usaidizi wa mawasiliano.
- Uthibitisho wa uzoefu na/au uwezo wa kusambaza na kubandika taarifa za mawasiliano katika ukanda wa kati katika mikoa ya Kagera, Geita, Tabora, Shinyanga, Singida, Dodoma, Manyara na Tanga ikihitajika.
- Uwezo wa kifedha kuweza kutoa huduma zinazohitajika ikiwa ni pamoja na kuwasilisha mahesabu ya fedha ya mwaka 2020.
- Inashauriwa, mwonyesha nia atume maombi ya kusajiliwa na kanzi data ya EWURA (LSSP) kama mtoaji na msambazaji wa huduma ndani ya nchi wakati wa kuwasilisha ombi la kuonesha nia ya kutoa usaidizi husika.
- Uzingatiaji wa Kanuni za Maudhui ya Wazawa za mwaka 2012 pamoja na tafsiri ya Kampuni ya Wazawa (Nafasi za Ajira na Huduma kwa Watanzania).
- Usajili stahiki kutoka kwa mamlaka za nchi zinazohusika kwa ajili ya kutoa huduma stahiki inapobidi.
- Uthibitisho wa usajili katika Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) pamoja na Cheti cha Mwaka wa Karibuni cha Malipo ya Kodi.

Mashirika yenye nia ya kuleta maombi na ambayo yana uwezo na rasilimali za kutekeleza shughuli au kazi zilizoorodheshwa hapo juu yanapaswa kueleza nia yao pamoja na kuambatanisha pamoja na nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe kwa **eacop-tz.eoi.1000001@totalenergies.com** (ukubwa wa barua pepe usizidi 20 Mb) saa au kabla ya saa **11 jioni** za Afrika Mashariki (EAT) tarehe **11 Novemba 2021. Kichwa cha Baruapepe: 0010007126.**

**Muhimu:** Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na mashirika yatakayoonesha nia ili kutengeneza orodha ya Mashirika ya awali yenye vigezo vinavyotakiwa. Mashirika yatakayokidhi vigezo tu ndiyo yatapokea na kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA) pamoja na mwaliko wa kuwasilisha zabuni katika kuendeleza mchakato wa zabuni. Maelezo yote ya kuonesha nia yanapaswa kuandikwa kwa lugha ya Kiingereza.

2165505

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

## LIMERUDIWA - OMBI LA KUONESHA NIA YA KUTOA HUDUMA ZA USAIDIZI KATIKA KITENGO CHA MAWASILIANO KATIKA MRADI WA BOMBA LA MAFUTA GHAFI LA AFRIKA MASHARIKI. KUMBUKUMBU: 0010007127

Kampuni ya Kimataifa ya Mafuta na Gesi ya TotalEnergies East Africa Midstream B.V, inaalika taasisi na kampuni zenye weledi na uzoefu katika Nyanja ya mawasiliano kuonesha nia ya kutoa huduma zinazohusiana na mawasiliano kwa Umma katika Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP).

Mradi wa EACOP unahusisha ujenzi na uendeshaji wa bomba litakalofukiwa chini ya ardhi litakalovuka mipaka ya nchi mbili na litakalosafirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Pwani ya Mashariki ya Tanzania kwa ajili ya kusafirisha mafuta hayo kwenda katika masoko ya Kimataifa. Bomba hili litaanzia Kabaale katika wilaya ya Hoima nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoani Tanga nchini Tanzania. Urefu wa Bomba ni kilomita 1,443, kati ya hizo, kilomita 1,147 zitakuwa Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI KUHUSU MAWANDA YA HUDUMA**

KAMPUNI inahitaji huduma za kampuni ya mawasiliano kutoa usaidizi katika moja au huduma mbalimbali tajwa kulingana na mahitaji:

- Sanaa ya kusanifu michoro, picha, miundo na alama kwa kutumia technolojia ya komputa (Graphics designing)
- Sanaa ya kusanifu miundo, picha na alama zenye mwendo, michoro yenye mwendo mfumo wa 2D &3D pamoja na michoro ya vielelezo kwa kutumia teknolojia ya komputa.
- Sanaa za jukwaani haswa katika maeneo ya mkuza wa bomba: Kagera, Geita,Tabora, Shinyanga, Singida, Dodoma, Manyara and Tanga.
- Huduma ya Kurekodi video zenye viwango vya juu pamoja na kuzihariri.
- Huduma za upigaji picha pamoja na uhariri wa picha.
- Huduma za kurekodi sauti ikiwemo kuzihariri.
- Tafsiri kutoka lugha ya Kiswahili kwenda Kiingereza na Kiingereza kwenda lugha ya Kiswahili hasa katika mfumo wa maandishi.

**VIGEZO MUHIMU:**

Makampuni au mashirika yatakayoonesha nia, yanaalikwa kutuma maombi pamoja na nyaraka zifuatazo:

- Uthibitisho wa uzoefu wa utendaji kazi bora pamoja na sampuli za kutekeleza kazi za usaidizi katika mawanda ya mawasiliano ya nia husika, kampuni au Taasisi inaweza kuonyesha nia kwa zabuni moja au zaidi kati ya zilizoorodheshwa hapo juu. Katika hatua hii, sampuli zote za kazi za mawasiliano zinatakiwa kuwasilishwa kupitia uzi wa taarifa (link) ambao hautarajii kuisha muda wake.
- Uthibitisho wa uwezo mfano kuwa na vifaa, miundo mbinu pamoja na muundo wa timu ya watendaji.
- Uthibitisho wa kufanya kazi katika miradi mikubwa yenye uhitaji mkubwa wa usaidizi wa mawasiliano.
- Uthibitisho wa uzoefu wa kufanya kazi katika ngazi za chini katika ukanda wa kati katika mikoa ya Kagera, Geita, Tabora, Shinyanga, Singida, Dodoma, Manyara na Tanga Sanaa za majukwaani utapewa kipaumbele.
- Uwezo wa kifedha kuweza kutoa huduma zinazohitajika ikiwa ni pamoja na kuwasilisha mahesabu ya fedha ya mwaka 2020.
- Inashauriwa, mwonyesha nia atume maombi ya kusajiliwa na kanzi data ya EWURA (LSSP) kama mtoaji na msambazaji wa huduma ndani ya nchi wakati wa kuwasilisha ombi la kuonesha nia ya kutoa usaidizi husika.
- Uzingatiaji wa Kanuni za Maudhui ya Wazawa za mwaka 2012 pamoja na tafsiri ya Kampuni ya Wazawa (Nafasi za Ajira na Huduma kwa Watanzania).
- Usajili stahiki kutoka kwa mamlaka za nchi zinazohusika kwa ajili ya kutoa huduma stahiki inapobidi.
- Uthibitisho wa usajili katika Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) pamoja na Cheti cha Mwaka wa Karibuni cha Malipo ya Kodi.

Mashirika yenye nia ya kuleta maombi na ambayo yana uwezo na rasilimali za kutekeleza shughuli au kazi zilizoorodheshwa hapo juu yanapaswa kueleza nia yao pamoja na kuambatanisha pamoja na nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe kwa **eacop-tz.eoi.1000001@totalenergies.com** (ukubwa wa barua pepe usizidi 20Mb) saa au kabla ya saa **11 jioni** za Afrika Mashariki (EAT) tarehe **11 Novemba 2021. Kichwa cha Baruapepe ni 0010007127.**

**Muhimu:** Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na mashirika yatakayoonesha nia ili kutengeneza orodha ya Mashirika ya awali yenye vigezo vinavyotakiwa. Mashirika yatakayokidhi vigezo tu ndiyo yatapokea na kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA) pamoja na mwaliko wa kuwasilisha zabuni katika kuendeleza mchakato wa zabuni. Maelezo yote ya kuonesha nia yanapaswa kuandikwa kwa lugha ya Kiingereza.

2165505

MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Bima ya Afya kwa wote iharakishwe

**JUZI** Spika Job Ndugai alihoji sababu za kuchelewa kwa uwasilishaji wa Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote bungeni na kuitaka serikali kuharakisha mchakato wake.

Sababu kubwa za kiongozi huyo kuhoji ni kwa sababu bima ya afya inagusa Watanzania wengi hususan wa kipato cha chini, na kwamba ni muda mwafaka kwa muswada huo kufikishwa kwenye muhimili huo ili itungwe sheria.

Aidha, alisema ni muhimu serikali ikasema kama kuna mkwamo mahali ili Bunge lisaidie, baada ya kufafanua kuwa zimetengwa Sh. bilioni 149 kwa ajili ya utekelezaji wa mpango wa bima ya afya kwa wote.

Hoja hii inarudi tena bungeni kwa mara nyingine kwa kuwa wakati wa Mkutano wa Bunge wa Mei mwaka huu, yalipowasilishwa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, wabunge walipaza sauti juu ya umuhimu wa bima ya afya kwa wananchi wote.

Aidha, walieleza namna wananchi wengi wanavyopata shida ikiwamo wengine kupoteza maisha kutokana na kutokuwa na bima ya afya, hivyo waliitaka serikali kuhakikisha inaupeleka bungeni Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote.

Hakuna anayeweza kubisha kuhusu umuhimu wa bima ya afya kwa kila Mtanzania, ndiyo maana nchi zilizoendelea suala la bima ni lazima na kila mwananchi anayo kwa ajili ya kumwezesha kupata huduma bora za afya, hatua iliyoongeza muda wa kuishi.

Tunaamini wapo wanaopoteza maisha kwa sababu hawana fedha za matibabu na iwapo wangekuwa na bima ya afya wangeendelea kuishi, lakini familia zimejikuta kwenye mzigo wa madeni kwa ajili ya kutafuta fedha za kugharamia matibabu kwa ndugu yao.

Wengine wameuza mali na hali huwa mbaya zaidi pale mtu anapofariki kwa kuwa familia hutakiwa kulipa deni kwanza ndipo wakabidhiwe mwili wa ndugu yao, matukio ambayo yanaongezeka licha ya kila hospitali kueleza kuwa kuna utaratibu wa kufuata ili kupata msamaha.

Iwapo mtu huyu angekuwa na bima ya afya maana yake angekuwa ameshajikusanyia fedha zinazomwezesha kugharamia matibabu, lakini kwa wale ambao wanalipia bima, lakini hawaugua kwa miaka mingi maana yake zinasaidia kugharamia matibabu ya wengine.


Kuna umuhimu mkubwa kuwa na Bima ya Afya kwa Wote kwa kuwa italeta manufaa makubwa kwa wengi kwa kuwa sasa nguvu kazi itakuwa na uhakika wa matibabu na kuwa na afya njema muda wote, maana yake watawajibika ipasavyo katika kutekeleza majukumu yao.

Tunaamini iwapo Muswada wa Sheria hii utawasilishwa bungeni, utakuwa umeshirikisha wadau wote muhimu kwa kutokana na umuhimu wa suala hilo na pia kutakuwa na ushiriki wa sekta binafsi.

Aidha, muswada huo ukifikishwa bungeni sasa utakuwa ni wajibu wa watunga sheria kuuangalia kwa jicho la uwakilishi wa wananchi wao, kwa kuhakikisha mambo yote ya msingi yamejumuishwa ili inapoanza kutekelezwa kama sheria rasmi kusiwe na changamoto au mkwamo. Hivyo, tunaona kauli ya Spika ya kuitaka serikali kuharakisha mchakato huo ni muhimu sana, tukiamini kuwa moja ya vipaumbele vya serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan ni afya za wananchi.

Tunaamini kuwa kila Mtanzania akiwa na bima itakuwa rahisi kwake kupata huduma za afya na kushiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo yake na taifa kwa ujumla. Ni imani yetu muswada huo ukifikishwa bungeni, wabunge watatekeleza wajibu wao kwa kuupitisha haraka, kwa kuwa wanaelewa vikwazo wanavyokumbana navyo wananchi wao katika kupata huduma za afya.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




Muungwana Lazima Nilonge



# Vigezo, masharti vizingatiwe maandalizi ya lishe kwa mtoto

Na Sabato Kasika

**KATIKA** miaka ya karibuni imezuka biashara ya unga wa lishe uliochanganywa na nafaka mbalimbali kwa ajili ya uji wa watoto, ambao umekuwa ukiuzwa madukani na hata wakati mwingine kutembezwa mitaani.

Vilevile, baadhi ya wazazi wamekuwa wakichukua mahindi, mchele, mtama, ulezi na karanga na kuvichanganya pamoja na kusaga kama unga wa lishe kwa ajili ya uji wa watoto wao.

Hata hivyo, wataalamu wa lishe wanashauri kuwa nafaka moja hasa ya mahindi, itumike kuchanganywa na vitu vingine, kwa kuwa ndiyo yenye viini lishe vingi kuanzia ganda la juu hadi kiini cha ndani.

Wanashauri hivyo, kutokana na kwamba mchanganyiko wa nafaka nyingi kwa ajili ya uji wa mtoto, unaweza kusababisha akapata choo kigumu na kwamba hayo ni madhara ya kiafya kwa mtoto mdogo.

Flora Mgimba, ni Ofisa Lishe wa Jiji la Dar es Salaam, anasema wazazi na walezi wengi wamezoea kuandaa unga kwa ajili ya watoto wao, wakichanganya nafasi za aina mbalimbali, jambo analolikiri kuwa kosa.

Kuna wengine wamezoea kununua unga wa lishe, badala ya kuandaa wenyewe kwa kuzingatia ushauri wa wataalamu wa afya, hali ambayo huenda inaweza isiwe salama kwa afya za watoto wao.

Ushauri wake ni kwamba, kuna haja ya kuwa na mchanganyiko katika tafsiri, kama mzazi ameandaa kilo mbili za wanga, basi aweke kilo moja ya protini na kwamba yaweza kuwa mahindi, ngano au mchele, kisha ukachanganywa na kilo moja ya karanga.

Anasisitiza kuwa uandaaji wa uji lishe unahitaji umakini na nafaka lazima ikauke vizuri, kwa kuwa unga huo unahitaji uzoefu na ufahamu vyema wa lishe. Kimsingi, pasipo umakini unaweza kuhatarisha afya ya mtoto husika.

Binafsi ninaamini kwamba mtu akipata mtoto ni safari mpya kwa wazazi wanaoanza kupitia na hubadilisha maisha na mipango yao, ili kumhudumia huyo Malaika wa Mungu. Hivyo, ni wazi umakini ni muhimu katika kuandaa chakula chake.

Lishe bora inalenga kuepusha watoto kupata utapiamlo ambao wataalamu wa lishe wanasema, unatokana na ulaji duni usiokidhi mahitaji ya mwili na kila mzazi anajitahidi kuwaandalia lishe bora kwa ajili ya mtoto wake.

Kwa maana hiyo, mchakato wa kumpatia chakula sahihi mtoto anayeanza kula ni moja ya jambo muhimu ambalo ninaamini kila mzazi anatakiwa kilihangaikia ili kuhakikisha mtoto wake anaendelea kuwa na afya bora tangu anapozaliwa.

Wataalamu wa lishe wanatafsiri ulaji unaopitiliza mahitaji ya mwili 'unaitwa lishe iliyokithiri.' Hivyo, suala la kuwa makini katika uandaaji chakula cha mtoto, unasisitizwa kumsaidia apate lishe inayohitajika mwilini.

Kwa kuwa wataalamu hao wanaweka wazi mahitaji ya mtoto anayeanza kupewa uji maalumu kama kianzio cha kujifunza kula, ni vyema ushauri wao ukazingatiwa kuepusha madhara ya kiafya.

Inaelezwa kuwa umri wa miezi sita, ndiyo sahihi kwa ambao mtoto huanza kupewa uji na kwamba yanatakiwa maandalizi mazuri yanayozingatia lishe bora, badala ya kufanya kwa mazoea namna ya kuandaa nafaka kwa ajili ya uji.

Ikumbukwe, lishe ni matokeo ya hatua mbalimbali kuanzia mckakato chakula kinapoandaliwa, kuliwa, kinasagwa, kinavyomeng'enywa na hatimaye kufyonzwa mwilini kujenga afya bora ya mwili.

Kwa mantiki hiyo, ndiyo maana wataalamu wa lishe wanasema lishe bora inatokana na kula vyakula vinavyokidhi mahitaji ya mwili kwa kiwango, lakini ubora na usalama wa chakula chenyewe.

Hivyo, ninaamini ni wakati mwafaka sasa wale waliozoea kurundika nafaka mbalimbali katika maandalizi ya uji, wazingatie ushauri wa wataalamu wa lishe ili watoto wao wasikumbane na tatizo la kupata choo kigumu.

# Samia mgeni rasmi miaka 50 Bugando

**Na Richard Makore,** MWANZA

RAIS Samia Suluhu Hassan anatarajia kushiriki kilele cha maadhimisho ya miaka 50 ya Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Bugando yatakayofanyika Novemba 18, mwaka huu, jijini hapa.

Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali hiyo, Dk. Fabian Masaga, aliyasema hayo jana jijini hapa katika kambi maalumu ya kutoa huduma za tiba za kibingwa na kibobezi bure kwa wananchi wa mikoa ya Kanda ya Ziwa.

Alisema maadhimisho hayo ni muhimu katika sekta ya afya na kwamba wameona wamwite kiongozi wa kitaifa ili kushiriki naye pamoja.

Dk. Masaga aliongeza kuwa Rais Samia amekuwa mstari wa mbele katika kuipa kipaumbele sekta ya afya kwa kujenga zahanati, vituo vya afya, hospitali na kuhakikisha dawa zinapatikana muda wote.

"Kutokana na umuhimu huo, Novemba 18, mwaka huu, tutakuwa naye Mheshimiwa Rais ili kushiriki katika maadhimisho hayo muhimu," alisema.

Dk. Masaga alisema kwa siku tatu mfululizo, wananchi watapatiwa bure uchunguzi wa magonjwa mbalimbali na kupatiwa matibabu na wengine kupewa rufani za kwenda Bugando.

Alisema idara zote zinazotoa huduma za matibabu Bugando, zimehamia mtaani katika viwanja vya Furahisha ili kuwasaidia wananchi ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya kusherehekea miaka 50 tangu kuanzishwa kwa hospitali hiyo.

Baadhi ya huduma za bure zinatolewa katika viwanja hivyo ni uchunguzi wa macho, moyo, figo, shinikizo la damu, viungo, magonjwa ya watoto, wanawake na magonjwa mengine kwa kadri mgonjwa atakavyojieleza kwa daktari.

"Madaktari wote bingwa na wabobezi wapo hapa na wanamsikiliza mgonjwa na kumfanyia uchunguzi, hivyo ni fursa kwa wananchi kufika katika viwanja vya Furahisha na kupata huduma za kibingwa na kibobezi bure," alisema.

Katika kambi hiyo ya matibabu, mgonjwa Veronica Mwita (30), mkazi wa jijini Mwanza ambaye ameugua kwa miaka minane na kushindwa kupata huduma kutokana na kukosa fedha, jana alifikishwa hapo na kufanyiwa uchunguzi bure.

Mgonjwa huyo alifikishwa katika kambi hiyo akiwa amebebwa mgongoni na dada yake na kufanyiwa uchunguzi na madaktari waliobobea na kisha kupewa rufani kwenda Bugando.

Akizungumza na Nipashe, mgonjwa huyo aliishukuru Hospitali ya Bugando kwa kuanza kufanyia vipimo kwa kuwa ameteseka kwa miaka minane kwa kukosa matibabu kutokana na kukosa fedha.

Alisema mwaka 2013 alianza kuumwa na kwamba ameangaika katika hospitali kadhaa, lakini alikwama kuendelea katika hospitali ya Bugando kutokana na kukosa fedha.

Alisema anasumbuliwa na tumbo, figo na sasa miguu imekufa ganzi na kumfanya ashindwe kusimama wala kutembea.

Veronica mwenye watoto wawili, alisema baada ya kuumwa alikimbiwa na mume wake na kwamba hivi sasa anaishi na mama mkwe wake eneo la Buswelu jijini Mwanza ambaye anampatia chakula.



Mwenyekiti wa Bodi ya Makandarasi (CRB), Mhandisi Consolata Ngimbwa (katikati), akifungua mkutano wa makandarasi mkoani Iringa jana. Wengine ni Meneja wa CRB Kanda ya Kusini, Mhandisi Ally Mwita (kushoto), Mratibu wa Mafunzo, Neema Fuime (wapili kushoto), Mwezeshaji wa mafunzo hayo, Prof. Honest Ngowi (kulia) na Naibu Msajili CRB, David Jere. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Makandarasi wasisitizwa umakini mikataba

**Na Joseph Mwendapole,** IRINGA

MAKANDARASI nchini wametakiwa kusoma mikataba kwa umakini kabla ya kutia saini ili kuepuka kuingia kwenye mikataba ambayo wanaweza kushindwa kuitekeleza na kukimbia miradi wakati wa kuitekeleza.

Hayo yalisemwa jana mjini hapa na Mwenyekiti wa Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB), Consolata Ngimbwa, wakati akifungua mafunzo ya siku tatu kwa makandarasi wazalendo wa Nyanda za Juu Kusini kuhusu usimamizi wa biashara. Mhandisi Ngimbwa alisema ni vyema mkandarasi akajiridhisha na mkataba anaoingia kwa kuusoma vizuri na kama haelewi, kuomba ufafanuzi ili asijiingize kwenye mkataba ambao hataweza kuutekeleza.

Alisema baadhi ya makandarasi wamekuwa wakiwapa watu hasa wahandisi kuwajazia zabuni hali ambayo imesababisha wakose zabuni hizo kutokana na kujazwa bila kufuata taratibu.

"Msiwape watu wengine wawajazie na mkipata zabuni msome mikataba kwa umakini. Msikimbilie kusaini (kutia saini) tu mwishowe mnalalamika kumbe yale mliyolalamikia yalikuwapo wakati unatia saini," alisema "Unakuta kwenye zanuni umeambiwa ueleze uzoefu wa miaka mitano wewe unajaza uzoefu wa miaka mitatu halafu unasubiri upate zabuni na ukikosa unalalamika wakati hukukidhi vigezo," alisema Mhandisi Ngimbwa.

Aliwataka makandarasi kuungana ili kuwa na nguvu ya kutekeleza miradi mikubwa ya ujenzi kwani hata kampuni kubwa za Wachina zimekuwa zikiungana kwa ajili ya kutekeleza miradi mikubwa.

Makandarasi wengi, alisema wamekuwa wakiogopa kuingia kwenye kufanya kazi kwa ubia kwa kuhofia kupata hasara lakini alisisitiza kuwa ubia haukwepeki kwa kuwa ndiyo jawabu la mafanikio ya makandarasi wazalendo.

"Kazi za ubia zina chanagamoto zake lakini msiogope kufanyakazi kwa umoja kwasababu ukiwa kwenye ubia kuna mambo mengi unajifunza na unapata uzoefu wa kutosha kufanya miradi mikubwa," alisema

Aliwataka pia kuachana na utaratibu wa kuwa na vyama vingi vya makandarasi na kuanzisha chama kimoja chenye nguvu ambacho kitakuwa sauti yao wanapokuwa na matatizo mbalimbali kwa serikali au kwa wateja wao. Pia aliwataka makandarasi kujifunza kujaza zabuni kwa kutumia mfumo wa kielektroniki wa serikali wa TANePs ambao ndio unatumika kwa sasa kujaza zabuni za serikali.

Meneja wa CRB nyanda za juu kusini, Mhandisi Ally Mwita, alisema wateja wanapaswa kuwalipa makandarasi kwa wakati ili waweze kutekeleza miradi wanayopewa kwa wakati uliopangwa na kwa ufanisi.

"Umempa mkandarasi zabuni ametumia fedha zake na amekamilisha unapaswa kumlipa kwa wakati ili na yeye alipe wanaomdai na kushindwa kufanya hivyo ni kumdhoofisha mkandarasi" alisema

# Wachimbaji wadogo walia na uhaba vifaa

**Na Elizabeth John,** MBEYA

WACHIMBAJI wadogo wa madini Chunya mkoani Mbeya, wamesema wanakabiliwa na ukosefu wa vitendea kazi ambavyo wamedai wamekuwa wakivipata kwa shida sambamba na bei za kemikali kwa ajili ya uchenjuaji wa madini.

Mwenyekiti wa wachimbaji madini mkoa wa Mbeya, Leonard Manyesha, alisema hayo juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari wanawake 32 kutoka vyombo mbalimbali wanaofanya ziara ya kutangaza vivutio vya utalii na uwekezaji ikiwa ni sehemu ya kumuunga mkono Rais Samia Suluhu Hassan.

"Serikali ikitutatulia hizo changamoto nadhani uzalishaji wetu unaweza ukawa maradufu kulinganisha na ilivyo sasa. Ningeomba serikali itambue na ituelewe wachimbaji wote nchini na kutufanyia utafiti maeneo yetu yawe muhimu ili tuchimbe tupate dhahabu," alisema Manyesha.

Mwenyekiti huyo pia alisema madini yanaruhusu watu wote kuingia kwenye shughuli za uchimbaji kwa kutumia mifumo ya kimtandao ya namna ya upatikanaji wa leseni.

"Unaweza ukawa Mwanza au nje ya nchi, unaweza ukawa Mtwara au popote pale ukatafuta eneo lililo wazi katika Wilaya ya Chunya na unaweza ukapata eneo ukachukua msimbo ukalipia leseni yako. Sisi wawekezaji hatuwatengi kwa sababu ujio wa wawekezaji hawa wanatupa maarifa ya kupata uelewa mkubwa zaidi wa kiuchimbaji wa madini. Hii inatufaa sana kwa sisi kwa hiyo wawekezaji nchini tunawakaribisha sana mkoa wa Mbeya," alisema.

"Tumeshajipanga tuna shirikisho la wachimbaji nchini ambalo limewezesha masoko, tuna uchimbaji ambao hausumbui na mpaka sasa hivi matokeo ya uchimbaji nchini umewezesha kuchangia upatikanaji mkubwa wa mapato ya dhahabu," alisema.

Katika ziara hiyo, waandishi wa habari hao walitembelea uwekezaji wa shule, viwanda na hoteli ambako wawekezaji walisema nchi imeweka mfumo mzuri wa uwekezaji licha ya changamoto ambazo zinaweza kutafutiwa ufumbuzi.

# Serikali yaweka mapendekezo ukomo wa bajeti trilioni 39.3/-

**Na Gwamaka Alipipi,**
DODOMA

SERIKALI imeweka wazi Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa kwa mwaka 2022/23, kwamba kiwango cha ukomo wa bajeti kwa mwaka huo kinachokusudiwa ni Sh. trilioni 39.387.

Kiwango hicho ni ongezeko la Sh. trilioni 2.707 ya iliyokuwa mwaka 2021/22 ya Sh. trilioni 36.681, sawa na ongezeko la asilimia 7.4.

Kwa mujibu wa mapendekezo ya mwongozo wa maandalizi ya mpango wa bajeti ya serikali kwa mwaka 2022/23, uliosomwa jana bungeni , Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, alisema maakadirio hayo ni sawa na asilimia 22.4 ya Pato la Taifa.

Mwigulu alisema kuwa katika muda wa kati, matumizi ya serikali yanakadiriwa kuongezeka kwa wastani wa asilimia 5.9 kwa mwaka hadi Sh. trilioni 43.52 mwaka 2024/25.

Maeneo yanayotarajiwa kuwa na matumizi makubwa ni pamoja na mahitaji ya Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ikijumuisha ulipaji wa deni la serikali, kugharamia mishahara ya watumishi wa umma, pamoja na miradi mikubwa ya maendeleo inayoendelea.

Pia, ilieleza kuwa katika muda wa kati, serikali itaendelea kutoa msukumo katika kutekeleza vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 - 2025/26).

Waziri Mwigulu alivitaja vipaumbele hivyo kuwa ni kuchochea uchumi shindani na shirikishi, kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji huduma, kukuza biashara na uwekezaji pamoja na kuchochea maendeleo ya watu na kuendeleza rasilimali watu.

Ilieleza kuwa serikali itahakikisha sera za mapato na matumizi katika muda wa kati zinajikita katika kutekeleza vipaumbele vilivyoainishwa.

VIPAUMBELE

Waziri Mwigulu alisema katika mwaka 2022/23, maeneo yatakayopewa kipaumbele ni pamoja na kugharamia miradi ya kielelezo inayoendelea, Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022, deni la Serikali, mishahara ya watumishi na huduma za jamii zikiwamo afya, elimu na maji.

Kuhusu makadirio ya mapato ya ndani yakijumuisha mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, ilieleza kuwa yanakadiriwa kuongezeka hadi Sh. trilioni 28.56 kutoka makadirio ya Sh. trilioni 26.3.

Kadhalika, ilieleza kuwa katika kipindi cha muda wa kati, mapato yanakadiriwa kukua kwa wastani wa asilimia 7.3 na kufikia Sh. trilioni 32.56 mwaka 2024/25.

"Mchango wa mapato ya ndani katika bajeti unakadiriwa kuongezeka kutoka asilimia 71.9 mwaka 2021/22 hadi asilimia 72.5 mwaka 2022/23 na kuongezeka hadi asilimia 74.8 mwaka 2024/25," alisema Waziri Mwigulu.

Aidha, alisema kuwa mapato ya ndani kwa Pato la Taifa yanakadiriwa kuwa wastani wa asilimia 16.2 katika muda wa kati. Alisema kuwa katika mwaka 2022/23, mapato yanayokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) (kodi na yasiyo ya kodi) yanakadiriwa kuongezeka kwa asilimia 7.9 hadi Sh. trilioni 24.237 kutoka makadirio ya Sh. trilioni 22.471 mwaka 2021/22.

Kadhalika, alisema katika muda wa kati, mapato yasiyo ya kodi (wizara, idara, taasisi na Mamlaka za Serikali za Mitaa) yanakadiriwa kuongezeka kutoka Sh. trilioni 3.913 mwaka 2021/22 hadi Sh. trilioni 4.330 mwaka 2022/23 na kuongezeka kufikia Sh. trilioni 4.855 mwaka 2024/25.

Alisema kuwa mapato hayo yanakadiriwa kukua kwa wastani wa asilimia 7.5 katika muda wa kati.



Rais wa Hoteli za Golden Tulip Afrika, Alain Sebah (katikati), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, wakati wa uzinduzi wa ujenzi wa hoteli ya nyota tano itakayojengwa jijini Dodoma. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Asilimia 25 magonjwa moyo chanzo tumbaku

**Na Mary Geofrey**

MKURUGENZI Mtendaji wa Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI), Prof. Mohamed Janabi, amesema kati ya wagonjwa 100 wanaougua moyo 25 kati yao chanzo ni matumizi ya tumbaku.

Aidha, amesema takwimu zinaonyesha kuwa watu milioni nane hupoteza maisha kila mwaka duniani kutokana na kuathiriwa na matumizi ya tumbaku.

Alitoa takwimu hizo jana jijini Dar es Salaam, wakati akizungumza katika mkutano wa Chama cha Kudhibiti Matumizi ya Tumbaku nchini (TTCF) kupitia ripoti ya utafiti unaohusu jinsi mataifa yanavyolinda sera za afya dhidi ya kuingiliwa na sekta ya tumbaku inayoonyesha kuwa Tanzania inaendelea kudorora.

Prof. Janabi alisema asilimia 25 ya wagonjwa wote wa moyo ni wale ambao wanavuta au wanaoishi na watu wanaovuta sigara.

Akizungumzia uwiano wa magonjwa ya moyo na Uviko-19, alisema yote yanashambulia mfumo wa upumuaji.

"Sigara zinamwathiri anayevuta na aliye karibu na anaye vuta, mke, mume au watu wanaokuzunguka na ubaya zaidi watu milioni nane hupoteza maisha kila mwaka na wakati Uviko-19 watu milioni tano ndiyo wamepoteza maisha duniani," alisema Prof. Janabi.

Vile vile, alisema utafiti unaonyesha asilimia 80 ya wagonjwa wanaougua saratani chanzo chake ni matumizi ya tumbaku.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa TTCF, Lutgard Kagaruki, alisema kila mwaka watu 14,700 hufa kutokana na magonjwa yanayozuilika yanayosababishwa na tumbaku.

Aliiomba serikali kupandisha bei za sigara ili kudhibiti matumizi ya bidhaa hizo kwa kuwasilisha bungeni muswada wa kudhibiti tumbaku unaokidhi matakwa ya Mkataba wa Kudhibiti Tumbaku wa Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO, FCTC).

"Bei za sigara zipo chini sana kulinganisha na mataifa mengine, naiomba serikali ipandishe bei kwa sababu wavutaji ni vijana na watu maskini hawatamudu gharama na matumizi yatapungua," alisema Lutgard.

Kadhalika alisema huduma zinazohusiana na matumizi ya tumbaku zipigwe marufuku kama ilivyopendekezwa katika mkataba huo ili kuhakikisha uwazi kwa maofisa wa serikali utakaosaidia kurekodi mwingiliano wowote na sekta ya tumbaku pale itakapokuwa lazima.

Alisema pia uchambuzi wa gharama na faida wa biashara ya tumbaku unaonyesha hasara zaidi kwenye mazingira na afya kuliko manufaa yoyote ambayo hudanganya kuleta katika uchumi.

# Airtel, Precision Air zazindua tiketi mtandao

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya simu za mkononi Airtel, imeingia ubia na kampuni inayotoa huduma za usafiri wa anga nchni, Precision Air, kwa kuzindua promosheni mpya itakayowawezesha wateja wake watakaolipia tiketi za usafiri wa kampuni hiyo, kufurahia punguzo la asilimia tano kupitia Airtel Money.

Airtel Money na Precision Air walitangaza kuanza kwa promosheni hiyo maalum jana kwa kuwapatia wateja wa Precision Air urahisi katika kupanga safari zao na kuwawezesha kununua tiketi wakati wowote kupitia huduma hiyo ya fedha kwa njia ya mtandao.

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo, Mkurugenzi wa Airtel Money, Isack Nchunda, alisema: "Ushirikiano wetu tunaotangaza leo (jana) utawaongezea wateja wetu wa Airtel urahisi na uhakika wakati wa kulipia safari zao za ndani na za nje kwa kufanya malipo kidigitali pale wanapohitaji tiketi wakiwa popote.

"Kupitia ofa hii mpya, wateja wetu watafanya malipo ya tiketi zao za ndege kupitia huduma ya Airtel Money kisha mteja atapata punguzo la asilimia tano ya pesa aliyolipia tiketi hiyo."

Alisema ujio wa makubaliano haya unadhihirisha dhamira ya Airtel kutoa huduma bora za malipo kidigitali na kuwahakikishia wateja unafuu zaidi kwa kuwarejeshea fedha hizo ili wazitumie kufanya mambo mengine.

Naye Mkuu wa Biashara wa Precision Air, Lilian Mremi, alisema ushirikiano huo umekuja wakati muafaka kwa kuwa kampuni hiyo imejipanga zaidi kuwahudumia wateja kwa kufanya huduma za usafiri wa anga kuwa za kipekee.

"Wateja wetu sasa wanaweza kufanya malipo ya tiketi zao za ndege kupitia huduma ya Airtel Money. Hii maana yake ni kujihudumia mwenyewe kupitia simu yako ya mkononi. Mteja unaweza kutembelea tovuti yetu kufanya 'booking' ya safari kisha kulipia kupitia Airtel Money na kupokea tiketi yako ya kielektroniki kupitia simu yako ya mkononi," alisema.

Kuhusu namna ya kupata huduma hiyo, Meneja Uhusiano wa Airtel, Jackson Mmbando, alisema huduma hiyo ni rahisi kutumia kwa kuwa mteja anachotakiwa kufanya ni kufanya 'booking' ya safari au kufanya 'booking' kupitia tovuti ya Precision Air. Baada ya kufanya hivyo, alisema mteja atapewa namba ambayo itatumika kama kumbukumbu wakati wa malipo kwa ajili ya kununua tiketi. Pia alisema njia nyingine ni kuingia kwenye 'My AirtelApp' na kufuata utaratibu huo.

Alisema baada ya mteja kufanya hayo atapokea ujumbe wenye uthibitisho wa malipo na tiketi yake.

# 'EAC watekeleze uamuzi wa Mahakama ya Afrika'

**Na Gwamaka Alipipi**

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Mwinyi, ameshauri nchi za Afrika Mashariki kushirikiana kuchangia mafanikio ya Mahakama ya Afrika Mashariki na Haki za Binadamu na Watu, kwa kutekeleza ipasavyo uamuzi inaoutoa.

Rai hiyo ilitolewa juzi na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora Zanzibar, Haroun Ali Suleiman, alipozungumza kwa niaba ya kiongozi huyo wakati wa ufunguzi wa mkutano wa utekelezaji na athari za uamuzi wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu jijini Dar es Salaam.

Alisema hatua hiyo itawahakikishia walalamikaji mbele ya mahakama matunda ya kesi zao, lakini itaonyesha dunia nzima kwamba nchi za Afrika sasa zinachukulia kwa uzito ulinzi na uendelezaji wa haki za binadamu.

Alisema kuwa mwaka huu mahakama hiyo inatimiza miaka 15 tangu ilipoanzishwa ikiwa na mafanikio mengi katika kulinda haki za binadamu ingawa inakabiliwa na vikwazo mbalimbali.

Alisema anaamini kuwa mkutano huo wa siku tatu unafanyika katika muda mwafaka kwa kuwa washiriki watajadili na kuibua hoja nzito za namna bora ya kumaliza vikwazo mbalimbali vinavyoikabili mahakama hiyo.

"Mahakama hii ni taasisi yetu, tuliianzisha wenyewe. Ninaamini hili ni jukumu letu sote Waafrika kuhakikisha taasisi hiyo haishindwi kufikia malengo yake.

"Ninathubutu kueleza kuwa hakuna faida kwa Afrika ikiwa mahakama hii itakuwa imeshindwa au haitoi mchango katika ulinzi na ukuzaji wa haki za binadamu kote Afrika," alisema.

Rais wa Mahakama hiyo, Imani Aboud, alisema baada ya mkutano huo, mahakama hiyo inategemea washiriki watakubaliana njia bora zaidi za kuboresha kazi na majukumu.

"Huwa tunasema mnapokutana na kuzungumza mnapata mwafaka wa pamoja katika masuala ambayo yanaleta vikwazo na kikwazo kikubwa tulichonacho ni utekelezaji wa uamuzi wa Mahakama ya Afrika.

"Ndiyo maana tumewaita wadau wote muhimu ili tuzungumze ni vikwazo gani ambavyo wao wanaviona vinawakwamisha katika kutelekeza uamuzi wa mahakama," alisema.

Alibainisha kuwa wakati mahakama hiyo inasherehekea miaka 15 tangu kuanzishwa kwake, ni uamuzi mmoja kati ya 10 uliotekelezwa na nchi wanachama.



Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa (katikati), akikata utepe kuzindua vifaa vipya vya kazi vyenye thamani ya Sh. bilioni 210, jijini Dar es Salaam juzi, kwa ajili ya kurahisisha shughuli za Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA). **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Ulega ataka wafugaji wakorofi wadhibitiwe

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, amesema wafugaji wanaoingiza mifugo yao kulisha katika mashamba ya wakulima ni wahalifu kama wahalifu wengine, hivyo ni lazima wachukuliwe hatua za kisheria.

Ulega aliyasema hayo jana wakati wa ziara yake ya kutatua migogoro ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi aliyoifanya wilayani Mkuranga, mkoani Pwani.

"Ikiwa mtu amevamia shamba la mwenzie na mifugo yake ikala mazao katika shamba hilo, hapo hakuna kupindisha maneno. Ni lazima haki itendeke, achukuliwe hatua za kisheria ikiwamo kumfidia yule ambaye mazao yake yameliwa na mifugo," alisema Ulega.

Waziri Ulega alitumia nafasi hiyo pia kuvitaka vyombo vya ulinzi na usalama kufanya kazi ya dhati kabisa kusimamia utatuzi wa migogoro hiyo kwa nia ya kutunza amani na utulivu katika wilaya hiyo na nchi kwa ujumla.

Pia aliushauri uongozi wa wilaya kuunda kamati maalum za maridhiano zitakazoshughulika na utatuzi wa migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi ili watu wakae kwa amani na kushirikiana.

Ulega alimtaka Mkuu wa Wilaya ya Mkuranga, Hadija Nasir, kuratibu mpango wa kuwatoa wafugaji katika maeneo ambayo hayakupangwa kwa ajili ya shughuli za mifugo na kuwapeleka katika maeneo yaliyopangwa kwa ajili ya kazi hiyo.

"Sisi wizara tumekusudia kufanya mapendekezo makubwa na tumeshakubaliana kuandaa na kupeleka mapendekezo kwa mamlaka za juu kuomba maeneo ambayo yatapangwa na kuwekewa miundombinu kama maji na majosho kwa ajili ya mifugo ili wafugaji waondoke katika maeneo ambayo yanawakutanisha na nyie wakulima," alisema.

Mbali na mipango hiyo ya serikali ya kutenga maeneo, Waziri Ulega aliwataka wafugaji kuanza kupanga mikakati ya kuvuna mifugo yao ili waanze kupata faida ya kipato, lakini pia itasaidia kupunguza migogoro baina yao na watumiaji wengine wa ardhi.

"Hapa zitakuja Sh. milioni 200 za kutengeneza mnada wa Chamgoi utakaowawezesha wafugaji kuvuna mifugo ili kunufaisha halmashauri, taifa na wafugaji wenyewe," alibainisha.

Awali, wakulima wanaofanya shughuli zao katika wilaya hiyo akiwamo, Amiri Katundu wa kijiji cha Dondo Dutani na Ramadhani Kingu wa kijiji cha Kizapala, kwa nyakati tofauti walisema wafugaji waliovamia wilaya hiyo wamewasababishia athari kubwa katika mashamba yao ikiwamo kukosa mavuno ya kutosha kwa sababu mifugo imekula mazao yao.

Mkuu wa wilaya hiyo alisema kutokana na changamoto zilizojitokeza za uvamizi wa wafugaji, wameshaanza kuchukua hatua mbalimbali za kudhibiti migogoro kati ya wafugaji hao na watumiaji wengine wa ardhi ikiwamo kufanya operesheni za kudhibiti uingiaji holela wa mifugo katika wilaya hiyo.

## Namtumbo yaongoza uchanjaji chanjo Uviko

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

WILAYA ya Namtumbo, mkoani Ruvuma inaongoza kwa kuchanja wananchi wake kwa asilimia 100 chanjo ya Uviko-19 aina ya Sinopharm.

Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo, Lucia Kafumu, alisema sababu kubwa ya kuchanja wananchi wengi wilayani humo ni uelewa walioupata kuhusu elimu iliyotolewa na wataalamu wa afya, viongozi wa serikali, dini na ushirikiano na wananchi wenyewe kwa wenzao.

Kafumu alisema wakati timu ya wataalamu wa afya inapita kutoa elimu katika vijiji kwa njia ya mikutano ya hadhara ilipata ushirikiano wa viongozi wa serikali, viongozi wa dini, chama na baadhi ya wananchi ambao walijitokeza kuelimisha wenzao.

Vile vile, kitendo cha viongozi wa serikali kutoka katika vijiji vya Wilaya ya Namtumbo kujitokeza kuchanja kimesaidia wananchi wengi kujitokeza kupata chanjo baada ya kuona viongozi wao wanachanja.

Mratibu wa Chanjo Mkoa wa Ruvuma, Wilbroad Mvile, alikiri kupokea maombi ya dozi 500 za chanjo ya Sinopharm na tayari zimetolewa kwa Wilaya ya Namtumbo kwa ajili ya kwenda kugawa kwenye vituo vya kutolea huduma ya afya katika halmashauri ya wilaya hiyo ili uchanjaji usisimame.

## NMB, Britam sasa zawapa wavuvi bima

**Na Mwandishi Wetu,** MWANZA

BENKI ya NMB kwa kushirikiana na Kampuni ya Bima ya Britam wamezindua bima maalum ijulikanayo kama Jahazi kwa ajili ya kuwasaidia wavuvi katika mikoa mbalimbali.

Bima hiyo iliyozinduliwa jijini Mwanza na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, inalenga kutoa nafasi kwa wavuvi kupata kinga wanapopata majanga mbalimbali.

Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara wa NMB, Filbert Mponzi, alisema bima hiyo inawalenga wavuvi wadogo na wa kati, na kwamba wavuvi watakata bima ya asimilia 3 ya chombo husika cha shughuli ya uvuvi na kwamba wataweza kukingwa na majanga ya ajali, kuungua mitumbwi ama boti pamoja na watu watakaokuwa ndani ya vyombo hivyo.

Aliongeza kuwa faida nyingine za bima hiyo ni pamoja na familia ya mvuvi ama mtu aliyekuwa ndani ya chombo hicho kupewa mkono wa pole endapo kutatokea kifo pamoja na kupata ulemavu wa kudumu.

Aidha, bima hiyo itatoa gharama za matibabu kwa mvuvi pamoja na kulipwa fidia kutokana na ajali yoyote itakayompata atakapokuwa majini kwa ajili ya shughuli za uvuvi ama kando kando ya ziwa, mto, bwawa ama bahari.

Meneja wa Kampuni ya Bima ya Britam Kanda ya Ziwa, Said Kadabi, alisema bima hiyo itawasaidia wavuvi katika kuinuka kiuchumi kwa kuwa sasa watafanya kazi zao kwa kujiamini.

Alisema wanalenga kuyafikia makundi mbalimbali ya kijamii na kuyakatia bima ikiwamo mamalishe ili waweze kufanya shughuli zao kwa kujiamini zaidi.

Waziri Ndaki aliwataka wavuvi kutumia fursa hiyo kukata bima ili iwasaidie kuwakinga wanapokumbwa na majanga mbalimbali. Alisema siku za nyuma bima ilikuwa inawaangalia wavuvi wakubwa pekee na kwamba kwa sasa NMB na Britam wamekuja na aina mpya ya kuwasaidia wavuvi wadogo na wa kati.

# Serikali yaagiza kulipa malimbikizo yote madai ya watumishi wa umma

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais Utumishi na Utawala Bora, Mohamed Mchengerwa, amewaagiza wakurungezi wa wizara na halmashauri nchini kuhakikisha wanalipa malimbikizo yote ya madai ya watumishi.

Aidha, amesema tangu kuingia madarakani Rais Samia Suluhu Hassan, serikali imelipa malimbikizo ya madai ya watumishi mbalimbali kiasi cha Sh. bilioni 138.

Mchengerwa, alibainisha hayo jana jijini hapa wakati alipokuwa akitoa taarifa ya wizara yake kwa vyombo vya habari kuhusu mafanikio yaliyopatikana kwa kipindi cha miaka 60 ya Uhuru wa Tanganyika.

Alisema, pamoja na kutoa kiasi hicho cha fedha kwa ajili ya kulipa malimbikizo ya madai ya watumishi pia Rais Samia, hivi karibuni ametoa kiasi kingine ambacho serikali bado inafanya uhakiki wa madai ili kuanza malipo.

"Kumekuwapo na malalamiko kwa muda mrefu ya malimbikizo ya madeni ya watumishi, lakini kupitia serikali ya awamu ya sita chini ya Samia Suluhu Hassan, ameweka mikakati ya kuhakikisha watumishi wote wanaodai wanalipwa sitahiki zao," alisema Mchengerwa.

Vilevile, alisema dhamira ya serikali ni kuhakikisha kuwa inarudi katika mstari kwa kuhakikisha kuwa watumishi wote wanaostahili kulipwa wanalipwa, lakini wanao stahili kupanda madaraja wanapanda pamoja na kupandishwa kwa mishahara yao.

Akizungumzia kuhusu vitendo vya rushwa kwa watumishi wa umma, alisema taifa haliwezi kupiga hatua kama vitendo hivyo vitaendelea kupewa nafasi katika ofisi mbalimbali.

"Rushwa ni adui wa haki hatuwezi kuendelea kama rushwa itaendelea kupewa nafasi kila mmoja wetu anatakiwa kwenda kuzuia vitendo vya rushwa," alisisitiza.

Akizungumzia mafanikio yaliyopatikana katika miaka 60, tangu uhuru alisema ni pamoja na kuongezeka kwa ajira katika utumishi wa umma kutoka watumishi 17,565 mwaka 1961 hadi 528,290 mwezi Oktoba, 2021.

"Kati ya hao watumishi wa sekta ya afya wamefika 72,961 sawa na asilimia 13.8 na walimu wamefika 281,729 sawa na asilimia 53.3," alisema.

Alisema mafanikio mengine ni pamoja na kuboresha mfumo shiriki wa taarifa za kiutumishi na mishahara (HCMIS) na kujengewa uwezo wa watumishi kutoka taasisi za serikali za 427 kutumia mfumo huo.

"Pia kuwaondoa kwenye orodha ya malipo ya mishahara watumishi 15,578 waliobainika kughushi vyeti vya kufaulu mtihani wa kidato cha nne, cha sita na ualimu kati ya watumishi 535,770 waliohakikiwa," alisema.

Alisema pia wamewaondoa katika orodha ya malipo ya mishahara watumishi 5,335 walioajiriwa katika utumishi wa umma kinyume na sifa za miundo ya maendeleo ya kiutumishi.

Kadhalika alisema wamewaondoa katika orodha ya malipo ya mishahara watumishi hewa 19,708 na kuiwezesha serikali kuokoa jumla ya Sh. bilioni 19.84.

"Tumeimarisha mfumo wa kitaasisi wa usimamizi wa serikali mtandao kwa kuanzisha sheria ya serikali mtandao namba 10 ya mwaka 2019 na kanuni zake za mwaka 2020 zinazoweka utaratibu na masharti ya kisheria kuhusu utekelezaji, usimamizi na uendeshaji wa serikali mtandao nchini," alisema.




Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa (USAID) Tanzania, Kate Somvongsiri (katikati), akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya kinamama waliohudhuria katika halfla iliyoandaliwa na mradi wa USAID Tulonge Afya kupitia jukwaa la NAWEZA, mkoani Kigoma juzi, wenye lengo la kuwakutanisha kinamama wenye watoto chini ya miaka 5, kujadiliana masuala mbalimbali yanayohusu afya ya mama na mtoto ili kuwapa uzoefu wa jinsi ya kuwalea watoto wawe na afya njema. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ndugai aita viongozi NIDA wajieleze kusuasua utoaji Vitambulisho vya Taifa

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, ameiagiza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje kuwaita viongozi wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), wajieleze kwa nini utoaji vitambulisho bado unasuasua.

Alitoa agizo hilo jana bungeni na kueleza kuwa NIDA wamekuwa wakisuasua katika kazi zao, wanapaswa kuhojiwa katika kamati hiyo, ili Watanzania wajue hatima ya vitambulisho vyao.

"Kamati ya Mambo ya Nje waiteni NIDA, tumeanza nao kitambo hawa, lakini ni kiswahili tu, ninyi kamati ndiyo mtatuambia ukweli kuhusu kupatikana kwa vitambulisho," alisema Ndugai.

Spika Ndugai alilazimika kutoka agizo hilo baada ya Mbunge wa Makunduchi, Ravia Idarus Faina, kuhoji bungeni kwa nini uzalishaji wa vitambulisho umekuwa ni wa kusuasua licha ya serikali kuwaongezea mashine zingine mbili.

Katika swali la msingi mbunge huyo alihoji, ni lini serikali itajenga Ofisi za NIDA katika Wilaya ya Kusini Unguja. Akijibu swali hilo, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Khamisi Hamza Chilo, alisema kazi ya kuzalisha vitambulisho inaendelea vizuri baada ya kuongezwa kwa mashine za kuzalisha.

Chilo alisema hadi Oktoba 12, mwaka huu NIDA walikuwa wamezalisha zaidi ya vitambulisho 10,000 ambavyo vinasubiri kusambazwa kwa wananchi.

Alibainisha katika kutekeleza mpango huo, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) imefanikiwa kufungua ofisi 150 katika wilaya zote za Tanzania Bara na Zanzibar.

"Mheshimiwa Spika, Ofisi ya NIDA katika Wilaya ya Kusini Unguja itajengwa katika mwaka wa Fedha 2022/2023," alisema Naibu Waziri huyo.

Serikali imenunua mashine mpya yenye thamani ya Sh. bilioni 8. 5 kwa ajili ya kufyatua vitambulisho vya NIDA.

Kwa mujibu wa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, mashine hiyo ina uwezo wa kutoa vitambulisho 9,000.

## PURA ilivyomwaga ajira kwa wazawa

**Na Elizabeth Zaya**

MAMLAKA ya Udhibiti Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA), imesema imefanikisha lengo lake la kutoa ajira kwa wazawa katika kipindi cha utekelezaji wa mradi wa utafutaji wa data za mitetemo za 3D kwenye kitalu cha Ruvu na miradi mbalimbali inayotekeleza kwenye maeneo mbalimbali nchini.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Kitengo cha Ushirikishwaji wa wazawa na uhusishwaji wa wadau(LCSEU) wa PURA, Charles Nyagi, mamlaka hiyo imejipanga kuhakikisha Watanzania wananufaika zaidi katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya shughuli za mkondo wa juu wa petroli zinazoendelea nchini.

"Kipaumbele hiki si tu kwa nafasi za ajira, bali hata manunuzi ya huduma na bidhaa zinazohitajika wakati wa utekelezaji wa miradi, mafunzo, uhaulishaji wa teknolojia na uwajibikaji wa kampuni husika kwa jamii zinazozunguka miradi," alisema Nyagi.

Meneja Rasilimali Watu wa kampuni kandarasi ya mradi huo, BiTengwu, alisema tangu kuanza kwa mradi huo Machi hadi Oktoba mwaka huu, Watanzania 530 wamepata nafasi za ajira kwenye mradi huo huku wafanyakazi wa kigeni wakiwa ni 31.

Alisema walioajiriwa kwa kazi za ujuzi ni 18, ujuzi wa kati 220 na katika nafasi za ujuzi wa chini ni 292 na kwamba waajiriwa kutoka nchini China kwa nafasi za ujuzi ni 27 huku Wakenya wakipatiwa nafasi nne za ujuzi wa kati.

"Sambamba na nafasi hizo za ajira, Watanzania waliofanya kazi kwenye mradi wamenufaika na mafunzo mbalimbali yaliyotolewa kwa lengo la kuboresha utendaji na kuwaongezea ujuzi kwenye utekelezaji wa mradi," alisema Tengwu.

"Baadhi ya mafunzo ambayo wafanyakazi hao wamenufaika ni pamoja na ya utaratibu wa uendeshaji wa operesheni za kimtetemo ambayo yalinufaisha wafanyakazi 314, mafunzo ya zimamoto pamoja mafunzo ya kujikinga na ugonjwa wa corona."

## TCCIA kufungua ofisi ndogo Dodoma

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

CHEMBA ya Wafanyabiashara wenye Viwanda na Kilimo Tanzania (TCCIA), inatarajia kufungua ofisi yake ndogo jijini Dodoma kama sehemu ya mikakati yake ya kufanikisha utekelezaji wa sera ya serikali ya kujenga uchumi wa viwanda ifikapo mwaka 2025.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kikao cha ndani cha Bodi ya Wakurugenzi wa Chemba hiyo, Rais wa TCCIA, Paul Koyi, alisema chemba ya chombo chenye mtandao mkubwa wa wafanyabiashara wenye viwanda na kilimo nchini imejipanga kwenda sambamba na kufanikisha azma ya serikali ya kujenga uchumi wa viwanda.

"TCCIA tayari tumeshaanza kutekeleza azma hiyo ya serikali ya kujenga uchumi wa viwanda ifikapo 2025 kwa vitendo. Na sasa tunatarajia Mheshimiwa Spika Job Ndugai atatufungulia ofisi ndogo ya chemba hapa makao makuu ili kuongeza ufanisi wa hazi za chemba," alisema Koyi.


Alisema ufunguzi wa ofisi makao makuu ni mongoni mwa mipango ya TCCIA ya kufanya mageuzi ndani ya chemba ikiwamo ufanisi wa utoaji wa huduma zake kwa wanachama na Watanzania kwa ujumla.

ama
ALHAMISI NOVEMBA 4, 2021
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 13

**ILICHORIPOTI NIPASHE JANUARI...**
**Hatimaye iliyokuwa kliniki chini ya mti kijijini, zahanati rasmi inakuja**



Ukurasa 12

**SIMULIZI KUTOKA TRAFIKI, TBS, WADAU...**
**Ushindi mkubwa wa ajali barabarani nchini unaoendana na hitaji la mengi**

# Kundi la maelfu mabinti, dada zao wakwepeshwa hatari VVU

## •Watafutiwa mbadala wasizurure mtaani



Mabinti wilayani Kahama, wakipata mafunzo ya kiufundi yanayowapa ujuzi wawe mbali na maradhi Ukimwi. **PICHA: SHABAN NJIA.**

**Na Shaban Njia, KAHAMA.**

MABINTI walioko katika umri kuanzia miaka 15 hadi 24, wengi wako katika mazingira hatarishi ya umaskini uliokithiri, huku wanatumika ulezi wa familia wanazotoka.

Wamekuwa wakihangaika kukabili makali ya maisha Hapo ndipo penye mwanzo wa mazingira hatarishi kukaribiana na maambukizi mapya ya ugonjwa Ukimwi, wakipoteza nguvu za uzalishaji.

Kuelemewa maisha, mara zote ni mwanzo wa kundi hilo kuingia katika maambukizi mapya ya maradhi UKIMWI. Ni bahati kwao wapo wadau wanaowezesha kufanikisha hilo.

Shirika lilsilo la kiserikali, hadi sasa limewawezesha kiuchumi mabinti walioko katika umri huo mgumu, pamoja na kundi la kinamama vijana jumla yao 84,000, wapate stadi za kujihami kukabili maradhi hayo.

Pia, imevuka kuwezesha mabinti katika umri mdogo kupata stadi za mafunzo ya maisha ikiwamo udereva na ufundi mbalimbali, kama vile; umeme, magari, uchomeaji, cherehani, kompyuta, saluni na urembo.

Ni mradi unaofadhiliwa na Mpango wa Dharura wa Rais wa Marekani wa kukabiliana na UKIMWI (PEPFAR) na shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa (USAID).

**WENYE MRADI**

Agnes Junga, Ofisa Mabinti Balehe na Kinamama Vijana kutoka shirika hilo, anasema ni mpango ya kujikwamua kiuchumi, ikiwa sehemu ya kukabili maambukizi mapya ya VVU.

Ofisa huyo anasema vijana hao wamewezeshwa kupitia mradi Epic unaotekelezwa kwa miaka mitano, ikihusishwa na Shirika la Maendeleo la Marekani (USAID), katika huduma zake nchini.

Anasema kuna jumla ya mabinti balehe na kinamama vijana 84,000, kati yao wapo 56,000 ambao ni theluthi mbili wamewezeshwa kiuchumi kupitia vikundi vya kukopesha.

“Katika Chuo cha VETA Isaka , Halmashauri ya Kahama, tuna mabinti balehe na kinamama vijana 30 wanaosomea ufundi wa umeme, magari, uchomeleaji, kompyuta,cherehani, saluni na urembo. Lengo ni mradi uwakinge na maambukizi mapya dhidi ya Virusi vya UKIMWI.

Anawataja mabinti hao ni waliomaliza darasa la saba na hawakupata nafasi ya kuendelea na masomo.

**WANUFAIKA MRADI**

Ester Obadia, wanufaika wa mradi aliyeko masomoni katika Mamlaka ya Mafunzo na Elimu Stadi (VETA), pamoja na wenzake 29 waliochaguliwa kupitia vikundi vya wasichana vinavyosimamiwa na mradi wa EpiC, wakiwa na matarajio kujiajiri baada ya mafunzo.

Anasema kabla ya kupewa nafasi kujiunga na chuo hicho kusomea ufundi umeme, alikuwa mtaani akijihisi hatari ya kupata VVU.

Mwingine katika kundi hilo ni Mary Edward, anayesema awali waliishi katika mazingira magumu na kusababisha kuingia kwenye tabia zilizohatarisha maisha yao.

Sasa anarejea mafunzo kwamba, yatawasaidia kujitegemea na kujiepusha na vishawishi vinavyowaingiza kwenye mazingira hatarishi ya ngono.

“Msituone hivi tulivyo kwa sasa, kwenye jamii tunazotoka walikuwa wanatuona watoto wasiokuwa na nidhamu, huku kipato chetu kikiwa duni, hivyo kutengeneza utegemezi kwa wazazi, hata wanaume. Lakini, kwa ujuzi niliyo nao nitakwenda kuonyesha mfano kwenye kazi halali,” anasema Mary Edward.

Sasa anaomba mafunzo yawanufaishe mabinti wengi walio katika umri wake, akiamini ni hali inayosaidia kudhibiti UKIMWI, hasa mabinti wanaoishi pembezoni mwa miji.

Sophia Joseph, anayesomea kompyuta, anakiri mafunzi yanampa umahiri katika stadi hizo na kufahamu fursa mbalimbali za kiuchumi ambazo baada ya kumaliza mafunzo, wanaweza kuzitumia kwa ajili ya kipato.

“Tunasoma kwa vikundi. Kundi letu tunakopa Sh.10, 000 kwa kila mwanachama, hali ambayo kama mwanachama ataifanyia kazi vizuri unaweza kupata faida ya Sh. 30,000 na hii ndio inatusaidia kupata fursa ya kupata fedha, tofauti awali,” anafafanua.

Anaeleza kujikinga na VVU, wanashauriwa na wataalamu kufanya ngono salama kwa kinga, hali ambayo awali hawakulitambua, wakawa katika hatari ziadi.

**MRATIBU MAFUNZO**

Mratibu wa Mafunzo hayo kutoka katika chuo, St. Francis Vocation Training Centre, Charles Maganga, analipongeza shirika kuona umuhimu wa kuthamini mabinti na kuwapeleka chuoni mafunzoni, yatakayowasaidia maisha ya baadae.

Anasema, ujuzi wanaowapatia mabinti hao unawapa uwezo wa kufanya kazi popote, kulingana na fani zao, ingawa bado kuna kikwazo kikubwa cha ajira pindi wanapohitimu.

AFYA

## SIMULIZI KUTOKA TRAFIKI, TBS, WADAU…

# Ushindi mkubwa wa ajali barabarani nchini unaoendana na hitaji la mengi

**Na Yasmine Protace**

SIKU ya kukumbuka wahanga wa ajali huwa inaadhimishwa kimataifa kila ifikapo Jumapili wiki ya tatu ya mwezi Novemba. Lengo ni kuwakumbuka waathirika wa ajali barabarani, kuenzi mamilioni waliopoteza maisha, pia waathirika mbalimbali.

Ni hatua inayoenda na kaulimbiu moja kimataifa inayozungumzia usalama wa barabarani. Hadi sasa, kunaelezwa kuwapo wahanga wengi wa ajali vijana wenye umri kati ya miaka mitano na 29.

Hata hivyo, kwa mwenendo wa ajali nchini, sasa kunatajwa kuwapo ishara njema barabarani, kwa namna zinavyopungua kwa kasi kubwa, kutokana na kazi kubwa ya elimu barabarani inayoendelea.



Picha halisi ya ajali ilivyo katika namna tofauti. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

**HALI YA MUHIMBILI**

Daktari Bitta Muhanuzi wa Hospitali ya Taifa Muhimbili, anasema hivi sasa kuna ajali nyingi barabarani zinaongoza kuua watu wenye umri kuanzia miaka mitano hadi 29, akivitaja vifo vyake vinazidi maradhi vinara kama UKIMWI, kifua kikuu na malaria.

Dk. Muhanuzi anafafanua ajali bado zina nafasi kubwa kukabiliwa, hata kuzuiwa zisiendelee. Anafafanua asilimia 80 ya wanaofikishwa katika kitengo cha dharura hospitalini hapo wanalazwa na asilimia 20 waliobaki wanaruhusiwa kurudi.

Pia, ana ufafanuzi mwingine kuwa robo ya wagonjwa waofikishwa hapo wanatokana na ajali, nusu yake (asilimia 50.7) ni zao la ajali za pikipiki, huku idadi inayofuata ni wanaoanguka kutoka minazi.

Dk. Muhanuzi anataja theluthi moja (asilimia 32 ya ajali) ni majeruhi watembea kwa miguu na wanaofuata ni bodaboda, huku ya ajali hizo zinahusishwa na ulevi wakati wa kuendesha gari.

Kwa mujibu wa daktari huyo, kundi la majeruhi hao wa ajali wanaofikishwa Muhimbili, kuna asilimia mbili wanaoshindwa kufunga mkanda wa kiti, huku asilimia 13 hawamudu kutembea.

Daktari Muhanuzi anagusia lingine kwamba, asilimia 85 ya majeruhi wanaopata ajali wanakuwa hawana bima ya afya, hata kusababisha madeni makubwa kwa hospitali, kwani historia inaonyesha zaidi ya nusu kati yao wanashindwa kulipa madeni hayo.

**KAMANDA WA TRAFIKI**

Mussa Manyama, askari kutoka Polisi wa Usalama Barabarani makao makuu, anasema ajali, vifo na majeruhi vinavyotokana ya usalama barabarani vinapungua, kwa kipindi kati ya mwaka 2019 hadi 2020.

Anasema pamoja na ukuaji uchumi pia kuongezeka pato la taifa, hali iliyochangia ongezeko la usafiri, bado elimu ya kutosha haijawafikia madereva wa bodaboda wanaoendelea kujihusisha na makosa madogo.

Kwa mujibu wa Kamanda Manyama, hadi sasa Polisi imejipanga kuhakikisha matukio ya ajali yanaoungua na kufikia lengo la kutoweka.

Kamanda Manyama anatoa mfano katika kipindi cha kuanzia mwaka 2020, kulikuwapo ajali 978, zenye jumla ya vifo 616 na majeruhi 1128.

Lakini anasema katika mwaka uliofuata, idadi ya ajali ilishuka na idadi iloyopungua katika mabano kama ifuatavyo: 760 (218), zikiwa na idadi ya vifo 544 (72) na majeruhi 848 ambayo kuna upungufu wa 280 dhidi ya mwaka uliotangulia.

Kuhusu namna ilivyo suala la usalama barabarani, ni mtambuka na linapaswa kufanyiwa mabadiliko, ikiwamo madereva wasababisha ajali kuangaliwa, kwani binadamu anachangia asilimia 76 ya ajali zinazotokea.

Anarejea upande wa bodaboda, kinamama ndio waathirika wakubwa, kwani kwa kiasi kikubwa wanaoongoza kupata ajali kutokana kushindwa kuvaa kofia ngumu, wakihisi inawaharibia nywele kutokana na ama kusuka au kuremba kwa namna yoyote ile.

Kamanda Manyama anatoa mfano katika maeneo ujenzi barabarani unaendelea, unawachanganya madereva wengi kuwa visima vya ajali nchini.

**KAULI ZA WADAU**

Anold Majo, Ofisa Viwango kutoka Shirika al Viwango Tanzania (TBS), anasema viwango vya kimataifa vimeandaliwa mpaka katika sekta ya usafirishaji, hata kuanika viwango halisi na feki, ikiwamo 'kofia za lami.'

Anasema katika kuhakikisha hali ya usalama barabarani, wameanzisha dawati la malalamiko ambayo wananchi huwasilisha TBS malalamiko yao na yanafanyiwa kazi.

Pia, kuhusu umri sahihi ya kupanda Bodaboda, anataja ni mtoto kuanzia umri miaka 10 na zaidi na kuna kofia ngumu zinazoendana na saizi ya kichwa, hivyo kumuwezesha mtoto huyo kuvaa.

Anawataja wanawake wanaongoza kwa kutovaa kofia ngumu hiyo, wakihisi zinaharibu msuko wa nywele zao.

Injinia Mtufyo Mwakigonjwa, kutoka Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) mkoa wa Dar es Salaam, anasema ufinyu wa bajeti unachangia kutokafanyika kazi kwa kasi kubwa, akidokeza:

"Bajeti inatolewa ndogo, mtandao wa mahitaji ni mkubwa."

Anataja kingine ni kukosekana mizani kwa ajili ya kupimia vitu vizito barabarani huku kukiwapo baadhi ya waharibifu wakiwamo wezi wa vifaa vya barabara.

Mwakigonjwa anataja suala la uegeshaji magari katika maeneo yasiyofaa ,ujenzi holela na upitishwaji mifugo, uelewa mdogo wa wananchi katika matumizi barabara na uzembe wa madereva, wanaotengeneza magari barabarani yanapoharibika.

Florida Raymond, kutoka shirika la Mtandao na Vifaa, anasema shirika lao limefanikiwa kutembelea mikoa kadhaa kuzungumzia masuala ya usalama wa watoto.

Anasema Dar es Salaam, ni mkoa unaoongoza kwa matumizi ya vifaa vya watoto, hivyo wanaendelea kutoa elimu kwa jamii, ili waendelee kufahamu matumizi ya vifaa vya watoto katika magari.

Isabele Nchimbi, ofisa kutoka Chama cha Wanasheria Wanawake Tanzania (TAWLA), anafafanua lengo la kuandaa mafunzo hayo ni kuwafahamisha wanahabari masuala ya usalama barabarani, mkakati wake kwa jamii na kushawishi mamlaka kuboresha sheria za usalama barabarani, kwani hazijabadilika kwa miaka mingi.



AFYA

## ILICHORIPOTI NIPASHE JANUARI…

# Hatimaye iliyokuwa kliniki chini ya mti kijijini, zahanati rasmi inakuja

- Wananchi waanzisha, serikali ikawaitikia
- Diwani pekee mama aonyesha uchungu

**Na Dinna Maningo,TARIME.**



Kazi ya ujenzi wa zahanati kijijini Nyagisya, Tarime ikiendelea.

MTU anapofika kijijini Nyagisya katika kata ya Kiore, Wilaya ya Tarime, Mkoa wa Mara anakutana na neema ya kuwa na zahanati inayotokana na nguvu zao. Kwanini hiyo?

Ni zao la adha ya miaka nenda rudi, watoto na wajawazito kupata huduma ya kliniki chini ya mti, sambamba na kutembea mwendo wa kilomita mbili hadi 14, kwenda kuisaka zahanati ya Gamasara, Mtana na Hospitali ya Wilaya ya Tarime.

Ni uamuzi ulianzia kwa watu, pia kutumia nguvu zao, hapo ndipo Nipashe ilifika kijiji hapo jengo la vyumba 16 na choo lililojengwa kwa nguvu za wananchi.

Fundi ujenzi zahanati hiyo, Amos Lupiza, anasema boma hilo lina vyumba 16, ambavyo ni pamoja na chumba cha maabara, jengo la mama na mtoto, utawala, mapokezi na chumba cha kujifungulia

Ili kuwezesha mradi huo wa thamani Sh.17, 891, 500, mkazi Nyangi Ryoba anaiambia Nipashe kila aliyeoa amechanga Sh.14,000;wenye watoto ambao wako shule nao wamechanga 14,000.

Anafafanua:"Ambao hawakuchanga fedha ni wale wazazi ambao vijana wao wameoa na watu wote tumeshiriki kwenye maendeleo, tumechimba msingi wa maji kwa nguvu zetu."

Pia, katika makusanyo kuna fedha Sh. Milioni tano zilizotolewa na mbunge Mwita Waitara, kutoka Mfuko wa Jimbo Tarime Vijijini. Hatua iliyobaki iko mikononi mwa serikali kukamilisha baada ya kujengwa boma la zahanati.

**KUTOKA KIJIJINI**

Kaimu Mwenyekiti wa Kijiji cha Nyagisya, Ghati John, anasema sababu ya huduma kufanyika chini ya mti ni kuwapo mgogoro kati ya Kata ya Kiore na jirani zao, Manga.

John anaeleza wananchi wa kijiji Mtana walikuwa wakiwakataa majirani zao wa Nyagisya wasipate tiba kwao kwa madai wanasababisha wimbi kubwa la wagonjwa katika zahanati ya Mtana.

Diwani wa kata ya Kiore, Rhobi John, anatoa mchanganuo kuwa serikali ilishatoa fedha Sh. milioni 50; halmashauri Sh. milioni 15 na mbunge akachangia Sh. milioni tano.

"Ikikamilika, kata itakuwa na zahanati mbili ya Nyagisya na ya Nkerege, ambayo kutokana na jiografia yake wananchi wa Nyagisya wanalazimika kwenda kata ya Manga kupata huduma ya afya," anafafanua.

Hata hivyo, anaihimiza serikali kutoa msukumo unaofanikisa ujenzi wa mradi huo

**OFISA WA HALMASHAURI**

Ofisa Mipango wa Halmashauri ya Wilaya ya Tarime Frederick Mallya, anaiambia Nipashe wameshatenga bajeti Sh. milioni 50 kutoka serikali kuu za kujenga zahanati ya Nyagisya na Sh. milioni 10 kutoka mapato ya ndani ya halmashauri, zote zinalenga kufanikisha ujenzi tajwa.

Anasema halmashauri ina fedha Sh. milioni tano za fedha za Huduma kwa Kampuni kwa Jamii (CSR) ili kuchangia nguvu za wananchi wajengao boma la nyumba ya mtumishi wa Zahanati Nyagisya, ambazo zitatolewa ndani ya mwaka wa fedha uliopo.

Mnamo Januari 22 mwaka huu, gazeti hili lilchapisha hali halisi iliyopo kijijini hapo, huduma za kliniki kuendeshwa chini ya mti, wajawazito wanapimwa juu ya meza, uzito wa mtoto ananing'inizwa kwenye mti.

Serikali kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ilitoa tamko kuhusu huduma inayotolewa chini ya mti, kauli ya waziri mwenye dhamana, Dk.Dorothy Gwajima kutamka masikitiko hali ya huduma kufikia ngazi hiyo.

Pia, serikali mkoa wa Mara wilayani Tarime, wakiwamo wataalamu wa afya, aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Tarime, Mtemi Msafiri na aliyekuwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya Tarime, Apoo Tindwa, walifika kijijini kupata ukweli wa kilichoripotiwa ya huduma chini ya mti, ilipigwa marufuku na serikali.

**KAULI ZA WANAKIJIJI**

Nipashe ilipozungumza na wananchi kijiji hapo, wanasema sababu ya kujenga zahanati mahali hapo ni kukerwa umbali mrefu kufuata huduma ya afya inayosababisha baadhi ya wagonjwa, wajawazito na watoto kupoteza maisha baada ya kuchelewa matibabu.

Ester Chacha, anasema zahanati hiyo ikikamilika itakuwa msaada, kwani kupata kwao huduma ya kliniki chini ya mti na kwenye darasa, inawanusuru wagonjwa kupoteza maisha wanapokuwa wakitembea umbali mrefu kufuata huduma ya afya.

"Zahanati ikikamilika itatusaidia sisi akina mama ili ujifungue inabidi uchape mwendo kwenda zahanati ya Mtana. Kuna siku muda wa saa nane usiku bodaboda akiwa anatoka kumpeleka mjamzito kujifungua zahanati ya Mtana, wakati anarudi nyumbani akakutana na vibaka, ila aliwachenga akakimbia," anasimulia Chacha.

Msamba Machera anasema zahanati hiyo inapokamilika, itaepusha kero katika Mto Bukwe na Mto Kigera, kwani wakati wa mvua wanakijiji hushindwa kuvuka, maji kuwa juu ya daraja.

Machera anafafanua kwamba hata Siku ya Jumapili, wagonjwa huhangaika kupata usafiri wa pikipiki, waendesha pikipiki wanakuwa mnadani mjini Tarime kusaka abiria.

"Unaombwa Sh.10, 000 kwenda Mtana maana unakuwa umemtoa Tarime kukufuata wewe na anaweza kufika amechelewa, mgonjwa anafika kazidiwa wakati wa usiku usafiri wa pikipiki ni Sh. 30, 000,"anafafanua.

Mang'era Chacha anasema umbali kwenda kupata huduma ya kliniki katika Zahanati Mtana unawachosha kinamama, hata kulazimika huduma hiyo inatolewa chini ya mti na wakati wa mvua inahamishiwa darasani, katika Shule ya Msingi Nyagisya.

"Wagonjwa kwenye kijiji chetu wanapata shida huduma mpaka utembee zaidi ya kilomita nne, kwenda zahanati ya Mtana au zahanati ya Gamasara kilomita nne na wakati mwingine huduma unakosa na kulazimika kutembea kilomita 14 kuifuata Hospitali ya Wilaya Tarime," anasema ."Umbali huo ulituladhimu kuomba halmashauri itusogezee huduma ya klinikii (Mkoba) inayotembea," anasema na kuongeza, kijijini hapo hawakuona magari ya kiserikali kufika kukagua maendeleo, hadi pale habari hizo zilipoibuliwa na gazeti hili

Nyangi Ryoba anaiomba serikali kuharakisha ujenzi akiwa na madai: "Hapa kijijini pesa ni ya shida sana ili upate pesa mpaka uuze mazao au mifugo."

Mkazi Joseph Marwa, anafafanua si kwamba wananchi hawapendi kuchangia maendeleo kijijini, isipokuwa hawapati viongozi wahamasishaji.

Anampongeza Ofisa Mtendaji wa kijiji hicho, Waitara Kemo kwa bidii kuhamashisha maendeleo ya ujenzi wa zahanati.

Ghati Chacha anasema, kata ya Kiore imeongozwa na madiwani wanaume kutoka vyama tofauti kwa awamu tofauti, lakini aliyepo sasa mwanamama

Rhobi John, ameonyesha hamasa kubwa ya uchangiaji maendeleo, ikiwamo ujenzi wa zahanati.

"Huyu ndiye mwanamke pekee katika kata 26 za Halmashauri ya Wilaya ya Tarime aliyechaguliwa kwa kupigiwa kura na wananchi," Ghati anamsifu na kuongeza: "Ndiye anaujua uchungu wa mwanae. "



Ndivyo ilivyokuwa huduma ya kliniki ikiendelea kijijini Nyagisya, kutokana na ukosefu wa zahanati. **PICHA ZOTE: DINNA MARINGO.**

AFYA

# Mstaafu Diana: Ninateswa sana na yanayowakuta wenye familia pacha

- Abuni asasi kukabili madhila yanayowakuta
- Kisa? Aumizwa 'baba mapacha' kutapatapa



Diana Mbena akiwa amebeba mmoja wa watoto wa familia ya Fredrick Mwansasu, alipowatembelea katika makazi yao Kibaha, mkoani Pwani. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

**Na Sabato Kasika**

JAMANI mama fulani kajifungua watoto mapacha!.. hongera zake." Imezoeleka kusikika kauli hizo za pongezi kwa huyo aliyejaliwa, iwe watoto wawili au watatu.

Hata hivyo, ni wangapi wanafahamu magumu wanayopitia katika uzazi huo na sisi wapongezaji tuna msaada gani?

Ni majibu atakayoyapata baada ya tathmini, kama hayatamsukuma kuacha mdomo wazi, basi kuna nafasi kubwa ya kubaki anashangaa, ameshika tama...ni mabaya!

Hicho hasa ndicho kilichomgusa, Diana Mbena, mkazi wa Sinza Dar es Salaam, ambaye kiumri ni mstaafu na kijinsia mama. Anaumizwa na kinachoendelea, huku kila kona hashuhudii sura ya msaada kutoka kwa wahitaji.

Ameamua kuyakabili madhila hayo ya wazazi wasiokuwa na kosa, akitumia maisha yake ya ustaafu kutoka utumishi wa juu , baada ya kutumikia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), kwa kipindi cha miaka 22 kuanzia mwaka 1996 hadi 2018.

**NIKI KILICHOTOKEA?**

Diana anasema baada ya kustaafu, alinunua mashamba Kibaha mkoani Pwani na huwa anatafuta vibarua kumlimia, ili apande mazao mbalimbali katika mashamba hayo.

Mama huyo anasimulia: "Siku moja nilipokwenda shambani nilikutana na mwenyeji wangu akaniomba nimchukue kijana mmoja ambaye mke wake amezaa mapacha watatu awe miongoni mwa watakaolima."

Anafafanua kuwa taarifa aliyopewa ni kwamba kijana huyo anategemea kufanya kazi za vibarua, ndipo apate fedha za kununua mahitaji ya familia, ikiwamo chakula.

"Niliguswa sana na hali hiyo inabidi nianze kufuatilia maisha ya watu wanaojifungua mapacha kujua wanaishije, nikagundua kuwa wengi wao ni wale wa maisha ya hali ya chini, lakini hawajatambuliwa," anaeleza.

Anasimulia kwamba, familia zenye watoto mapacha huwa zinakabiliwa na vikwazo vingi, ikiwamo ukosefu wa lishe bora, matibabu na hata elimu sahihi.

> "Watoto wenyewe wana mwaka mmoja na miezi nane, wanahitaji chakula cha kutosha, hivyo ninawaomba wasamaria wema wengine zaidi wamuunge mkono mama Diana kutusaidia," anasema.

"Baadhi ya familia hizi zimekuwa zikikimbilia kwenye vyombo vya habari kutafuta msaada, pale mama anapojifungua watoto watatu au zaidi hapo na wakati mwingine wenza wao huwakimbia," anasema.

Diana anasema, suala la lishe bora ni muhimu kwa mama na watoto wake kwa ajili ya ubora wa afya zao na kwamba kwa mazingira ambayo baadhi ya wenye mapacha wanaishi, anaamini hawapati lishe bora.

**MZIZI WA UAMUZI**

Fredrick Mwansasu (42), anajitambulisha ndiye aliyesababisha Diana kuanzisha shirika hilo lililojikita katika kusaidia familia zenye mapacha.

Anasema, anaishi kwa kutegemea kazi za vibarua mashambani, myumbani akiwa na watoto mapacha watatu, hali inayomfanya kuna wakati anajikuta hana hata cha kuwezesha wanafamilia kula nyumbani.

"Mama huyo amekuwa msaada mkubwa kwa familia yangu, anatutumia fedha, akija huku lazima awe na kiroba cha unga, sukari mchele na nguo.

Pia, anatutia moyo katika maisha haya," anasema Mwansasu.

"Watoto wenyewe wana mwaka mmoja na miezi nane, wanahitaji chakula cha kutosha, hivyo ninawaomba wasamaria wema wengine zaidi wamuunge mkono mama Diana kutusaidia," anasema.

Mwansasu anafafanua kuwa, baada ya kupata watoto wawili, alikuwa amepanga na mkewe kuongeza wa tatu, lakini wakaja mapacha watatu, hivyo sasa wana jumla ya watoto watano.

Anasema kabla ya kwenda Kibaha, aliajiriwa kufanya kazi ya kukaanga chips eneo la Ubungo Dar es Salaam, lakini eneo walilokuwa wakilitumia likabomolewa, ndipo akachukuliwa kwenda kulinda shamba la mtu binafsi Kibaha.

**ALIANZISHIA SHIRIKA**

Mstaafu huyo anasema, mazingira hayo yalimsukuma kuanzisha shirika lisilo la kiserikali alilolipa jina la 'Eden Twins Foundation' lenye lengo kutangaza vikwazo vinavyowakabili watoto mapacha, ili jamii iwatambue.

"Pia, nimekuwa nikitafuta msaada kwa marafiki zangu, uwe wa nguo, chakula na fedha kwa ajili ya kuhudumia familia hizi ambazo matatizo yake hayajapewa uzito kama ilivyo kwenye matatizo mengine," anafafanua.

Diana anasimulia kwamba ameanzisha shirika lake Mei mwaka huu na ameandaa kinachoitwa 'Tamasha la Kutambua Watoto Mapacha', litakalofanyika Novemba 11 mwaka huu, jijini Dar es Salaam.

Anasema ameshatoa mwaliko kwa wadau wakiwamo viongozi wa serikali, pia sekta afya kwa ajili ya kuhudhuria tamasha hilo, ili kushirikiana nao kutoa maoni na jinsi ya kusaidia familia zenye mapacha nchini.

"Itakuwa ni nafasi ya pekee kwangu kuelezea yale yanazikabili familia zenye watoto hao, ili wajue zinapambana na vikwazo vingi na mwisho wa siku waniunge mkono katika juhudi hizo," anafafanua.

Mwenyekiti huyo anaeleza: "Ninatamani kukuza vipaji vyao, michezo kuwawezesha kuwa na maendeleo chanya, kuimarisha jamii juu ua uhifadhi wa mazingira, kuongeza ufahamu, kutambua na kukuza maslahi bora kwa mapacha ndani ya jamii."

**HITAJI LA LISHE LILIVYO**

Ofisa Lishe wa Jiji la Dar es Salaam, Neema Mwakasege, anatafsiri T mlo kamili unaotokana na chakula mchanganyiko kutoka makundi yote ya vyakula, kwa vile una virutubishi muhimu kwa ajili ya lishe na afya bora.

"Mlo huu unapoliwa kwa kiasi cha kutosha kulingana na mahitaji ya mwili angalau mara tatu kwa siku, huupatia mwili virutubisho vyote muhimu, lakini bahati mbaya wapo baadhi ya watu hawaupati," anasema Neema.

Anasema virutubishi ni viini vilivyoko kwenye chakula vinauwezesha mwili kufanya kazi zake mbalimbali na kwamba ulaji unaofaa hutokana na chakula mchanganyiko na cha kinachotosha.

"Lishe duni kabla na wakati wa ujauzito, inaweza kufanya watoto kuzaliwa na wakiwa na utapiamlo na hivyo kupunguza kinga ya mwili na kusababisha magonjwa ya mara kwa mara kwa mtoto," anasema.

Ofisa Lishe huyo anasema utapiamlo, pia huchangia kuongezeka vifo vya watoto na wajawazito, inapunguza ubora wa maisha na kufupisha umri wa kuishi, kuathiri maendeleo ya nchi na kupunguza uwezo wa kufanya kazi.





## Serikali yaagiza malipo watumishi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais Utumishi na Utawala Bora, Mohamed Mchengerwa, amewaagiza wakurugenzi wa wizara na halmashauri kuhakikisha wanalipa malimbikizo yote ya madai ya watumishi.

Pia amesema tangu kuingia madarakani Rais Samia Suluhu Hassan, serikali imelipa malimbikizo ya madai ya watumishi mbalimbali ya Sh. bilioni 138.

Mchengerwa alibainisha hayo juzi jijini Dodoma wakati alipokuwa akitoa taarifa ya wizara yake kwa vyombo vya habari kuhusu mafanikio yaliyopatikana kwa kipindi cha miaka 60 ya Uhuru wa Tanganyika.

Alisema pamoja na kutoa kiasi hicho cha fedha kwa ajili ya kulipa malimbikizo ya madai ya watumishi pia Rais Samia, hivi karibuni ametoa kiasi kingine ambacho serikali bado inafanya uhakiki wa madai ili kuanza malipo.

"Kumekuwapo na malalamiko kwa muda mrefu ya malimbikizo ya madeni ya watumishi, lakini kupitia serikali ya awamu ya sita chini ya Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, ameweka mikakati ya kuhakikisha watumishi wote wanaodai wanalipwa sitahiki zao," alisema Mchengerwa.

Pia alisema dhamira ya serikali ni kuhakikisha kuwa inarudi katika mstari kwa kuhakikisha kuwa watumishi wote wanaostahili kulipwa wanalipwa, lakini pia wanao stahili kupanda madaraja wanapanda pamoja na kupandishwa kwa mishahara yao.

Akizungumzia kuhusu vitendo vya rushwa kwa watumishi wa umma alisema taifa haliwezi kupiga hatua kama vitendo hivyo vitaendelea kupewa nafasi katika ofisi mbalimbali.

"Rushwa ni adui wa haki hatuwezi kuendelea kama rushwa itaendelea kupewa nafasi kila mmoja wetu anatakiwa kwenda kuzuia vitendo vya rushwa," alisisitiza.

Akizungumzia mafanikio yaliyopatikana katika miaka 60, tangu uhuru alisema ni pamoja na kuongezeka kwa ajira katika utumishi wa umma kutoka watumishi 17,565 mwaka 1961 hadi 528,290 mwezi Oktoba, 2021.

# CWT yalia malimbikizo nauli, uhamisho

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

CHAMA cha Walimu Tanzania (CWT), kimesema bado walimu wanakabiliwa na kero mbalimbali hususan za madai yasiyo ya mshahara na yatokanayo na mshahara na kuiomba serikali kulishughulikia suala hilo.

Hata hivyo, kimetaja mafanikio kadhaa yaliyopatikana tangu kuanzishwa kwake miaka 28 iliyopita ikiwamo kuwaondoa kwenye ajira za mitaani watoto 120 na kuwarejesha darasani.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini hapa kuhusiana na maadhimisho hayo, Kaimu Rais wa CWT, Dinnah Mathamani, alisema bado walimu wana madai kwenye suala la uhamisho na likizo.

Pia alisema kuna kero ya kutolipwa malipo ya bima ya maisha na Shirika la Taifa la Bima (NIC) na kuomba serikali kulifuatilia hilo kwa kuwa limekuwa kikwazo kwa walimu.

Alisema serikali ilishatoa maelekezo kuhusu uhamisho kwamba kabla mwalimu hajahamishwa, anatakiwa kupatiwa stahiki zake, lakini suala hilo halipewi kipaumbele na baadhi ya halmashauri.

"Tunawasiliana na wilaya mbalimbali walimu bado wana madai. Serikali imeshatoa maelekezo kuhusiana na suala hilo lakini utekelezaji bado ni shida," alisema.

Alizitaka halmashauri zote nchini zitenge fedha za uhamisho wa walimu na kuwapa malipo yao ya uhamisho kabla ya kuwahamisha.

Kuhusu suala la likizo, Mathamani aliiomba serikali isimamie suala hilo kwa kuwa walimu hawatendewi haki na baadhi yao hawapewi fedha zao kwa mujibu wa maelekezo.

"Tunaiomba serikali isimamie jambo hili utekelezaji wake haupo sawa, tena walimu wanapewa 'flat rate' yaani hajalishi mwalimu anatoka Dodoma kwenda Tabora au kwenda Bukoba wote unakuta wanapewa kiwango cha fedha za nauli kinacholingana," alisema.

Pamoja na hayo, aliwataka walimu kutekeleza wajibu kwa kufuata sheria, miongozo na maadili ya taaluma yao ili kujiepusha kuingia kwenye migogoro baina yao na waajiri wao.

Naye Katibu Mkuu wa CWT, Deus Seif, alisema tangu kuanzishwa kwa chama hicho mafanikio mbalimbali yamepatikana upande wa chama na wanachama na chama na mwajiri wake ikiwa ni pamoja na kuendelea kukaa meza moja na serikali kwa ajili ya kutatua kero zinazowakabili walimu.

Alisema majadiliano yao na serikali yamefungua wigo wa walimu kupanda vyeo.

Mweka Hazina CWT Taifa, alisema chama kimepata mafanikio mengi ikiwamo kujenga ofisi kila mkoa.

"Tumejenga majengo katika mikoa 20 na zaidi ya Sh. bilioni 20 zimetumika. Fedha hizi ni za wanachama na sasa hivi kuna ujenzi wa ofisi za wilaya na pia tunatarajia kujenga Makao Makuu ya CWT hapa Dodoma," alisema.



Mkuu wa Wilaya ya Dodoma Mjini, Jabir Shekimweri (kulia), akikabidhi kikombe cha ushindi wa kwanza kwa Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Chidachi, Veronica Suya (wapili kushoto), baada ya mwanafunzi wa shule hiyo, Joseph Thadei (kushoto), kuibuka mshindi wa shindano la kuchora picha zinaoonyesha mambo ya usalama barabarani, lililoandaliwa na Taasisi ya Amend kwa udhamini wa Kampuni ya Mafuta ya Puma Energy, jijini Dodoma juzi. Mwanafunzi huyo alizawadiwa 500,000/- na shule ilipewa Sh. milioni nne. Wapili kulia ni Mkaguzi Msaidizi wa Polisi, Leonce Kaimukirwa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Gwajima ataka ujenzi makao makuu ya wizara kwa wakati

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WIZARA ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, imepanga kukamilisha ujenzi wa jengo la ghorofa tisa ndani ya miezi 24 ambalo litakuwa na uwezo wa kuchukua watumishi 400 kwa awamu ya kwanza.

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, alibainisha hayo juzi wakati wa hafla ya kutia saini mkataba wa ujenzi katika eneo la mji wa serikali la Mtumba, jijini hapa.

Dk. Gwajima alisema makubaliano baina ya wizara na mkandarasi yametokana na serikali kutoa Sh. bilioni 23 kwa ajili ya ujenzi wa jengo hilo ambalo litajumuisha Idara Kuu Afya na Idara Kuu Maendeleo ya Jamii.

"Ni imani yangu kuwa mradi utaanza kwa wakati na kukamilika ndani ya miezi 24 kama ilivyopangwa.

"Hatutegemei kipindi cha miezi 24 kipite kama maelekezo ya serikali yalivyotaka halafu kazi iwe haijakamilika. Ni imani yetu mkandarasi atakuwa na mpango kazi utakaoainisha kila siku nini kitakuwa kinafanyika," alisema Gwajima.

Msanifu Majengo, Wencelaus Kizaba, kutoka Wakala wa Majengo Tanzania (TBA), alimhakikishia waziri kuwa watamsimamia mkandarasi ili kuhakikisha anakamilisha kazi hiyo ndani ya kipindi ambacho kimepangwa.

"Mheshimiwa Waziri, mkandarasi aliyepewa jukumu hili, anafahamika kwa sifa yake ya kuwa mkandarasi daraja la kwanza. Tuna imani kabisa kazi hii itakamilisha kwa wakati kama ilivyopangwa," alisema.

Mkandarasi Iqbal Singn, akizungumza kwa niaba ya Kampuni ya Nandhra Engineering and Constructions, alisema wanashukuru kwa kuaminiwa na serikali na kuahidi kwamba watahakikisha wanazingatia makubaliano ya mkataba na kukamilisha kazi kwa wakati.



# Upekee wa Hifadhi ya Ruaha wavutia watalii

**Na Grace Mwakalinga,** IRINGA

MAAJABU manne katika Hifadhi ya Taifa Ruaha yamechangia kwa kiasi kikubwa kuvutia watalii kutembelea na kujifunza aina mbalimbali za vivutio vilivyobarikiwa katika eneo hilo.

Maajabu hayo ambayo ndiyo upekee wa hifadhi hiyo, yanaifanya kuendelea kupokea watalii kila wakati ambao wanashawishiwa kushuhudia uzuri huo.

Ofisa Uhifadhi Utalii Hifadhi ya Ruaha, Amina Salum, akizungumza na Nipashe juzi alisema miongoni mwa vivutio vya kipekee katika eneo hilo ni uwezekano wa kuwaona kwa wakati mmoja wanyama 'lesser' na 'greater kudu' kwa sababu ni eneo la mtawanyiko kwa wanyama hao.

Aliongeza kuwa kuna uwezekano pia wa kuwaona swala aina ya palahala, korongo, tohe, nyumbu, mbwa mwitu, simba, duma, nyati, tembo pundamilia na twiga.

Alisema hifadhi hiyo imejaliwa kuwa na aina 574 za ndege wanaofanya makazi yao kwenye hifadhi hiyo na kuwa kivutio kikubwa kwa wageni kwa sababu utofauti wa uoto wa asili na mwinuko ndivyo visababishi vikuu kwa kuwepo kwa wingi wa aina tofauti za ndege hao.

"Kuwapo kwa utofauti mkubwa wa mwinuko kutoka mita 750 hadi 1868 huku kukiwa na Mto Ruaha Mkuu, mabonde na ardhioevu za Usangu, tambarare za juu na milima kama Isunkaviola na kingo za mgawanyiko ni sifa nyingine ya hifadhi yetu ya Ruaha," alisema Salum.

Alisema Hifadhi ya Ruaha inapatikana kwenye makutano ya mimea na wanyama kutoka upande wa kaskazini na kusini mwa Afrika, hivyo kuifanya kuwa na aina nyingi za wanyama na mimea.

Alisema uoto wa asili hutofautiana kutoka tambarare za Mto Ruaha ambapo ni nyika za wazi huku zikibadilika kuwa misitu ya miombo na kufikia kwenye kingo za tambarare zinazopatikana juu ya milima zikiwa na uoto tofauti kabisa huku bonde uevu la Usangu linatoa uoto wa kipekee hivyo kuwavutia wageni.

Alisema licha ya uwapo wa ugonjwa wa corona, wageni ndani ya nchi wamekuwa na mwitikio mkubwa kutembelea vivutio katika Hifadhi ya Ruaha kwa kutumia mbinu mbalimbali za kuhamasisha utalii kupitia vyombo vya habari na vipeperushi mbalimbali.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha, Halima Kiwango, alisema uhifadhi wa eneo hilo ulianza tangu mwaka 1910 wakati huo ikijulikana kama Pori la Akiba la Saba.

Alisema mwaka 1946 Waingereza waliongeza eneo na kubadili jina kuita Pori la Akiba la Rungwe na baadaye mwaka 1974 likatangazwa kama Hifadhi ya Taifa ya Ruaha.

Aliongeza kuwa Hifadhi ya Ruaha inafikika kwa njia ya barabara kilomita 108 kutoka mji wa Iringa ambayo inapitika mwaka mzima. Lakini pia kilomita 625 kutoka Dar es Saalam na kilomita 480 kutoka jijini Mbeya.



Mwakilishi wa watu wenye ulemavu ambao wanajihusisha na shughuli za uchimbaji madini mkoani Mbeya, Maria Mwasakali (kulia), akizungumza na waandishi wa habari jijini humo juzi, juu ya umuhimu wa elimu na matumizi ya nyenzo za kisasa za uchimbaji ambazo zitasaidia upatikanaji wa madini migodini baada ya kumalizika kwa warsha iliyoandaliwa na Shirika la Madini la Taifa (STAMICO). **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Waonya uuzaji mashamba holela

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WANANCHI katika Wilaya ya Mbeya wameshauriwa kuacha kuuza mashamba yao na badala yake wayapime na kumilikishwa kwa mujibu wa sheria ili kuyaongezea thamani.

Ushauri huo ulitolewa jana na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Mwalingo Kisemba, wakati akizungumza na Nipashe juu ya mikakati waliyo nayo katika kuwasaidia wakulima kunufaika na mazao wanayozalisha.

Alisema kumekuwa na tabia ya baadhi ya wananchi kuwauzia matajiri mashamba yao na kisha wao kubaki bila ardhi na wakati mwingine kuanza kukodishiwa na matajiri hao.

Alisema tatizo hilo litawasababishia umaskini kutokana na fedha wanazopata baada ya kuuza mashamba hayo kuzitumia kwa muda mfupi na kubaki mikono mitupu.

"Nawaombeni ndugu zangu msiuze mashamba yenu. Sasa hivi mji wetu wa Mbalizi unakua kwa kasi sana na serikali ina mpango wa kutuletea vyuo na viwanda vikubwa vya dawa, sasa haya maeneo yetu yatakuwa na thamani kubwa kuliko mnayoiona sasa hivi," alisema.

Alisema shamba lililopimwa na kumilikishwa kwa mujibu wa sheria huwa linakuwa na thamani na linaweza kumsaidia mwananchi kupata mkopo kutoka kwenye benki yoyote nchini.

Hivi karibuni Benki ya NMB ilizindua huduma mpya ya mkopo wa kuwasaidia wananchi kurasimisha makazi yao ambayo itawasaidia kupimiwa na kumilikishwa mashamba yao na kurejesha mkopo huo kwa muda wa miaka miwili.

# Milioni 180 hatarini kukumbwa na njaa

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

ZAIDI ya watu milioni 180 waishio nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara wanaweza kukumbwa na baa la njaa endapo shughuli za uzalishaji gesi joto zitaendelea.

Hata hivyo, ni asilimia nne tu ya uzalishaji gesi joto inayofanyika kwenye nchi za Jangwa la Sahara huku asilimia 96 ikizalishwa kwenye nchi zilizoendelea.

Kwa mujibu wa Mratibu wa Taasisi ya Green Faith International Tanzania, Baraka Lenga, ongezeko la mabadiliko ya tabianchi yanachangia uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara kupungua, hivyo kusababisha baa la njaa.

Kutokana na hali hiyo, Lenga alisema Mkutano Mkuu wa 26 wa Umoja wa Mataifa unaojadili masuala ya mabadiliko ya tabia nchi, ni muhimu sana kwa sababu unawaleta pamoja wafanyabiashara na wakuu wa nchi, wanaharakati na wanasiasa pamoja na taasisi zisizokuwa za kiserikali kujadili kwa pamoja ni kwa namna gani wanaweza kuepukana na mabadiliko hayo ambayo yanaweza kusababisha maafa kwa jamii.

Alisema mkataba wa makubaliano wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi, unalenga kuhakikisha jotoridi halipandi kuzidi kiwango cha digrii 1.5 na kwamba likienda mbali zaidi lisipande hadi digrii mbili.

Endapo jotoridi likienda zaidi ya hapo, alisema litaisababishia dunia kwenye matatizo makubwa kutokana ya kuingia kwenye wimbi la ukame na jangwa.

"Nchi 196 zilitia saini mkataba huo na kupatiwa majukumu ya kwenda kuorodhesha na kupambana na uzalishaji wa gesi joto ambazo ndio zinaharibu mfumo wa hali ya hewa na kusababisha mabadiliko ya tabia nchi. Katika mkataba huo ilionekana nchi nyingi zilizoendelea ndizo zinachangia kwa asilimia 96 ya mabadiliko ya tabia nchi huku nchi ambazo hazijaendelea zimechangia kwa asilimia nne," alisema Lenga.

Alisema mkutano unaoendelea ni wa muhimu sana kwa kuwa utatoa suluhisho la wapi tunaelekea sambamba na kupatiwa fedha kutoka nchi zilizoendelea ili kuhimili na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Mwaka 2018 katika Mkutano Mkuu wa 24 wa Mabadiliko ya Tabianchi, alisema wanasayansi walitahadharisha kuwa mabadiliko ya tabianchi yatasababisha watu zaidi ya milioni 122 kuingia kwenye umaskini katika kipindi kifupi kijacho.

Aliongeza kuwa uzalishaji wa chakula Kusini mwa Jangwa la Sahara utapungua kutoka asilimia 21 hadi asilimia tisa ifikapo mwaka 2080 kutokana na mabadiliko ya tabianchi.

Hata hivyo, Ofisa Maji wa Bonde la Ziwa Rukwa, Grace Chatanda, alisema miongoni mwa mikakati katika kuendeleza uhifadhi na vyanzo vya maji ni kutoa elimu kwa wananchi wanaozunguka maeneo hayo.

Alisema shughuli za kibinadamu zinachangia kwa kiasi kikubwa mabadiliko ya tabia nchi hivyo aliwaomba wananchi kuacha kufanya shughuli za kilimo, uvuvi na uchomaji misitu.



## Wanakijiji waridhia suluhu ya mgogoro

**Na Mwandishi Wetu**

WANANCHI wa Kijiji cha Michamvi Mkoa wa Kusini Unguja wameridhia uamuzi uliofanywa na serikali kuhusu mgogoro wa njia ya asili uliokuwapo kati yao na mwekezaji wa hoteli mpya ya kitalii inayojengwa kijijini hapo.

Waliyasema hayo katika kikao maalum kati yao na Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja aliyefika kijijini hapo kwa ajili ya kutafuta suluhu ya mgogoro kati ya wananchi na mwekezaji wa hoteli ya kitalii inayojengwa kijijini hapo.

Wananchi hao walisema maamuzi yaliotolewa na serikali wameridhika nayo na imeonyesha jinsi gani serikali inathamini wananchi wake katika kuyapatia ufumbuzi matatizo yanayowakabili.

Juma Mussa, alisema hatua ya serikali kuamua njia hiyo kutotumika kupita kwa vyombo vya moto na badala yake kutumiwa na wananchi kwa miguu na kufanya shughuli zao za kijamii kutasaidia kwa kiasi kikubwa kufanikisha harakati za maendeleo ikiwamo shughuli zao za uvuvi na kilimo cha mwani.

"Awali tulikuwa tunapata usumbufu mkubwa sana kutokana na ujenzi wa ukuta huu ambao ulisababisha kuziba njia ambayo tulikuwa tukitumia kwa ajili ya shughuli zetu za kimaendeleo ikiwamo kwenda baharini," alisema.

Naye Mkuu wa Mkoa Kusini Unguja, Rashid Hadidi Rashid, aliwataka wananchi wa kijiji hicho kuyaheshimu maamuzi hayo pamoja na kuendelea kuwa watulivu na kumpa ushirikiano mwekezaji huyo ili kulinda maslahi kwa pande zote mbili.

"Niwaombe wananchi kunapokuwa na tatizo msichukue sheria mikononi mwenu... ni vyema kuwasilisha malalamiko yenu katika sehemu husika ili kupatiwa ufumbuzi unaofaa," alisema Mkuu wa Mkoa.

Hivi karibuni wakazi wa kijiji hicho walivunja eneo la ukuta uliojengwa na mwekezaji na kusababisha mgogoro mkubwa kati yao na mwekezaji wa hoteli inayojengwa kijijini hapo.

**Wananchi hao walisema maamuzi yaliotolewa na serikali wameridhika nayo na imeonyesha jinsi gani serikali inathamini wananchi wake katika kuyapatia ufumbuzi matatizo yanayowakabili.**

# Mwinyi: Corona iliufanya mwaka wangu wa kwanza kuwa mgumu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema mwaka mmoja uliopita wa uongozi wake ulikuwa mgumu kutokana na nchi kukabiliwa na janga la ugonjwa wa corona.

Alisema ugonjwa huo umesababisha kushuka kwa utalii, pato la serikali, mzunguko wa fedha, kudorora na maisha kuwa magumu.

Aliyasema hayo jana wakati akiweka jiwe la msingi la ujenzi wa Hoteli ya L'Ousis huko Kizimkazi Mkoa wa Kusini Unguja.

Alieleza kuwa utalii unaendelea kuwa sekta mama ya uchumi wa Zanzibar, lakini kwa bahati mbaya corona imeathiri sana uchumi wa nchi.

Alisema kuwa hivi sasa ugonjwa huo umepungua na utalii Zanzibar umeanza kuimarika kwa kasi, hivyo imani yake kuwa uchumi utaimarika.

Alieleza kuwa wawekezaji wengi wamekuwa na imani ya kuwekeza Zanzibar kutokana na hali ya amani na utulivu iliyopo.

Alisema utalii unapaswa kuelekezwa katika mambo matatu ambayo yanapaswa kutekelezwa serikali za mikoa, Wizara ya Utalii na Serikali Kuu isiwe watazamaji tu. Alisema kwanza lazima wananchi wanufaike na utalii, hivyo alitaka uongozi wa Mkoa wa Kusini kuhakikisha wananchi wa Kizimkazi wananufaika na ajira ambazo zitatolewa na hoteli hiyo.

Alisema jambo la pili uongozi wa hoteli hiyo kuhakikisha unanunua bidhaa zinazotoka katika kijiji hicho ikiwamo samaki, matunda na mazao mengine yanayopatikana Kizimkazi.

"Hakuna sababu ya kuagiza bidhaa kutoka nje kwa zile ambazo zinapatikana kijijini hapa ili wananchi wetu kupata soko la kuuza bidhaa zao," alisema Dk. Mwinyi.

Dk. Mwinyi alisema jambo la tatu ni kuhakikisha uongozi wa hoteli unaimarisha huduma za kijamii katika vijiji vilivyoekeza hoteli hizo ikiwamo elimu, afya na barabara za ndani.

Naye Mkurugenzi wa hoteli hiyo, Ahmed Saber, alisema hoteli itakapokamilika itatoa ajira 300, na kwamba wazawa watapewa kipaumbele.

Alisema ujenzi wa hoteli hiyo ulianza Novemba mwaka jana na unatarajiwa kumalizika Machi mwakani na utagharibu jumla ya Dola za Marekani milioni 15.




Waziri wa Afya, Jinsia na Watoto Zanzibar, Nassor Ahmed Mazrui (kulia), akizindua Hospitali ya Dk. Mehta's katika Kijiji cha Paje, Kusini Unguja juzi. Kushoto ni mmiliki wa hospitali hiyo, Dk. Ameesh Mehta. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# SMZ yataka wawekezaji sekta ya afya

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Afya, Jinsia, Wazee na Watoto, Nassor Ahmed Mazrui, amesema Serikali ya Zanzibar imetoa nafasi kwa wawekezaji kuwekeza katika sekta mbalimbali ikiwamo ya afya.

Aliyasema hayo jana alipokuwa akifungua Hospitali ya Dk. Mehtas katika kijiji cha Paje Mkoa wa Kusini Unguja.

Alisema serikali itaendelea kuunga mkono jitihada zinazofanywa na wawekezaji wazalendo wanaowekeza sekta ya afya ambayo ina manufaa makubwa kwa wananchi wa Zanzibar.

Alisema serikali imetoa nafasi kwa wawekezaji kuwekeza hospitali binafsi na kujikita katika kufanya kazi na sekta binafsi katika kukuza uchumi wa Zanzibar.

Alisema moja ya nyenzo ya kukuza uchumi ni kuhakikisha wananchi, wawekezaji na wageniwanapatahudumabora za afya katika visiwa vya Zanzibar.

Alimpongeza mmiliki wa hospitali hiyo, Dk. Metha katika kuwasaidia wananchi, wawekezaji na watalii kwa kusogeza huduma bora za afya vijijini hasa katika ukanda wa utalii.

Aliwataka wakazi wa kijiji cha Paje na vijiji jirani kuitumia hospitali hiyo kupata matibabu kwa sababu huduma zake ni nafuu kwa wazawa.

Aidha, alipongeza hatua ya wawekezaji mbalimbali kuwekeza katika sekta ya afya na kwamba kwa sasa Zanzibar kuna hospitali binafsi 153.

Mazrui aliwataka wawekezaji wazalendo kufahamu kwamba wana wajibu wa kuwekeza nchini mwao na kuchangia masuala mbalimbali ya maendeleo.

Naye, Mwenyekiti wa hospitali , Dk. Ameesh Mehtas, alisema azma ya kuweka hospitali hiyo katika Mkoa wa Kusini ni kurahisisha upatikanaji wa matibabu sio tu kwa wakazi wa vijiji vilivyokuwapo katika mkoa huo bali pia kwa wageni wanaokuja nchini ili kuitangaza Zanzibar katika mataifa yao.

Alisema ni jukumu kwa Wazanzibari wote kushirikiana katika kuimarisha uchumi hasa kupitia sekta ya utalii.

"Mimi ni Mzanzibari ni mwananchi hivyo nimekuja hapa kujenga nchi yangu na nimeona umuhimu wa kusaidia sekta hii ya afya ili wananchi kupata huduma nzuri," alisema.

Duwa Suleiman Mussa, Mrajis wa hospitali binafsi, alisema hospitali binafsi zinasaidia sana waananchi katika kupata matibabu, hivyo aliwaomba wawekezaji ambao wanataka kuwekeza katika sekta hiyo kuzingatia misingi imara.

Aliwataka wawekezaji kuzidisha ujenzi wa hospitali binafsi na kutimiza vigezo vilivyoewekwa na serikali.

Akizungumza kwa niaba ya wakazi wa Kijiji cha Paje, Sheha wa kijiji hicho, Muhamed Rajab Makame, alisema kijiji hicho zaidi ya 4,000 na kina hoteli za kitalii na nyumba za kulala wageni 40, hivyo kufunguliwa kwa hospitali hiyo kutarahisisha upatikanaji wa huduma bora za afya.

# Watu tisa wauawa ghasia DRC

**Kinshasa,** DRC

GAVANA wa Jimbo la Kivu Kusini, Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), amesema watu tisa wameuawa katika operesheni ya kurejesha amani katika mji wa Bukavu.

Miongoni mwa watu waliouawa, ni watu sita ambao walifanya mashambulizi pamoja na askari wawili na polisi.

Watu 36 ambao walifanya uvamizi wamekamatwa, wakati uchunguzi ukiendelea. Ingawa hali ya maisha inaanza kurejea katika hali ya kawaida, baadhi ya maduka na ofisi zimeanza kufunguliwa tangu asubuhi. Askari wengi wamepelekwa kufanya doria katika mji huo.

Wakazi waliiambia BBC, walisikia milio ya risasi kuanzia majira ya saa saba usiku na wakabaki ndani hadi kulipokuchwa. Septemba mwaka jana viongozi wa wapiganaji wapatao sabini walisaini mkataba wa kusitisha mapigano DRC, serikali ilishindwa kuihusisha jeshi.

Aidha, makubaliano hayo hayakuweza kuleta amani katika eneo ambalo limekuwa na ghasia kwa miongo miwili, huko Kusini mwa Kivu. **BBC**

# Kenya: Mwanajeshi wa Uingereza arejeshwe kujibu tuhuma mauaji

**Nairobi,** KENYA

KENYA ina nia ya kuiomba Uingereza kumsalimisha mwanajeshi wa taifa hilo anayedaiwa kuhusika na mauaji ya mwanamke mmoja raia wa Kenya miaka tisa iliyopita.

Waziri wa Ulinzi Eugene Wamalwa, ameiambia kamati ya bunge kuwa serikali ya Uingereza imeahidi ushirikiano kamili.

Wamalwa alisema mwili wa Agnes Wanjiru, mwenye umri wa miaka 21, uligunduliwa baada ya wanajeshi wa Uingereza waliokuwa wakifanya mazoezi nchini Kenya kuondoka.

Wajumbe wa serikali ya Uingereza kwa sasa wapo nchini Kenya, wakifanya mazungumzo na wenzao wa Kenya, wamekataa maombi yote ya mahojiano na BBC.

Wamalwa aliwaambia wabunge Jumanne kwamba, alisoma ripoti ya uchunguzi iliyohitimisha kuwa Wanjiru aliuawa na wanajeshi wa Uingereza katika ardhi ya Kenya.

Aliongeza kuwa, serikali ya Kenya iliwasiliana na Uingereza baada ya taarifa ya Jumatatu ya mkuu wa polisi kwamba kesi hiyo, imefunguliwa tena.

Wamalwa pia alisema amepata hakikisho la serikali ya Uingereza kwamba, wale wanaosakwa kuhusiana na mauaji hayo, ikiwa wanajulikana, watafikishwa Kenya kujibu mashtaka.

**BBC**

# Ripoti yabaini uhalifu wa kivita Tigray

**Addis Ababa,** ETHIOPIA

PANDE zote kwenye mzozo wa Jimbo la Tigray, zimekiuka haki za kibinadamu, ukiukaji unaotajwa kuwa uhalifu dhidi ya binadamu, kwa mujibu wa ripoti mpya.

Mauaji ya kiholela, mateso, ubakaji na mashambulizi dhidi ya wakimbizi na watu waliohama makwao yote yametajwa.

Vita vilizuka Novemba 4 mwaka jana. Vilianza wakati Waziri Mkuu Abiy aliamrisha uvamizi dhidi ya vikosi vya jimbo la Kaskazini mwa Tigray.

Wanajeshi wa serikali wakati huo, waliwatimua waasi, mambo yalibadilika Juni wakati wapiganaji wa Tigray walipata mafanikio.

Kwa sasa wanaripotiwa kukaribia mji mkuu, Addis Ababa.

Siku ya Jumanne serikali ya Ethiopia ilitangaza hali ya hatari saa chache baada ya kutoa wito kwa wakazi wa mji mkuu kujihami.

Kamishna Mkuu wa Haki za Binadamu wa Umoja wa Mataifa Michelle Bachelet, alisema mzozo huo umekumbwa na ukatili mbaya na kutoa wito wa kusitishwa mapigano.

"Kuna sababu za kutosha kuamini kuwa pande zote katika mzozo moja kwa moja zilishambulia raia, au mali ya raia, kama nyumba, shule, hospitali na maeneo ya kuabudia au kufanya mashambulizi yaliyosababisha vifo vya raia na kuharibu mali ya raia," ripoti hiyo ilisema.

Ripoti hiyo inaeleza jinsi vijana kutoka Tigray wanaofahamika kama Samri waliwaua watu 200 kutoka jamii ya Amhara eneo la Mai Kadra mwezi Novemba mwaka uliopita.

Mauaji ya kulipiza kisasi kisha yakaendeshwa dhidi ya jamii ya Tigrinya katika mji huo huo.

Jeshi la Eritrea lilijiunga kwenye mzozo huo likiwasaidia wanajeshi wa serikali ya Ethiopia.

Wanajeshi wa Eritrea waliwaua zaidi ya raia 100 eneo la Axum kati kati mwa Tigray, Novemba mwaka jana, kulinga na ripoti hiyo.

"Uhalifu wa kivita huenda umetekelezwa kwa kuwa kuna sababu na kwa kuwa watu ambao hawakushiriki kwenye ukatili waliuawa na wale walioshiriki katika mzozo," ripoti ilisema.

Ripoti hiyo pia ilisema kuwa, kuna kesi za ukatili wa kingono ukiwamo ubakaji na kutoa wito kwa serikali ya Ethiopia kufanya uchunguzi kwa kutumia mashirika huru, kuhusu madai ya ukiukaji wa haki na kuwafikisha mbele ya sheria wahusika. **BBC**


EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

**OMBI LA KUONESHA NIA YA UTENGENEZAJI, UPIMAJI, USAMBAZAJI NA UTOAJI WA MABOMBA MAKUBWA YA HDPE**
**KUMBUKUMBU 0010007214**

Kampuni ya Kimataifa ya Mafuta na Gesi ya TotalEnergies East Africa Midstream B.V, inaalika taasisi zenye weledi na uzoefu kuonesha nia ya utengenezaji, upimaji, usambazaji na utoaji wa mabomba makubwa ya HDPE Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP).

Mradi wa EACOP unahusisha ujenzi na uendeshaji wa bomba litakalofukiwa chini ya ardhi litakalovuka mipaka ya nchi mbili na litakalosafirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Pwani ya Mashariki ya Tanzania kwa ajili ya kusafirisha mafuta hayo kwenda katika masoko ya Kimataifa. Bomba hili litaanzia Kabaale katika wilaya ya Hoima nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoani Tanga nchini Tanzania. Urefu wa Bomba ni kilomita 1,443, kati ya hizo, kilomita 1,147 zitakuwa Tanzania, ambapo bomba hilo litapita kwenye mikoa nane (8) ambayo ni Kagera, Geita, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Manyara, na Tanga; bomba la mafuta pia litapita kwenye Halmashauri za Wilaya 27 na vijiji 231.

**MAELEZO MAFUPI KUHUSU MAWANDA YA HUDUMA**

EACOP inahitaji huduma za mtengenezaji mwenye uzoefu na mwenye sifa nzuri kutoa huduma za utengenezaji, upimaji, usambazaji na utoaji wa mabomba makubwa ya ukuta wa HDPE kulingana na viwango na vipimo vilivyotajwa hapa chini:

**VIWANGO:**

Ukuta wa muundo wa Bomba za HDPE zitalingana kwa kuzingatia viwango EN 13476-2 / ISO 21138-2, na marekebisho yake, isipokuwa ikiwa imeainishwa vinginevyo.

**VIPIMO:**

- Kuta za kila sehemu ya HDPE (2.45m) zitalingana na vipimo vifuatavyo.
- ID / DN1500 na kipenyo ch nje cha ukubwa 1630 ± 10mm takriban idadi ya mita 400+ zinatakazowasilishwa katika sekesheni za mita 2.45.
- ID / DN1800 na kipenyo cha nje cha ukubwa 1960 ± 10mm takriban idadi ya mita 400+ zinatakazowasilishwa katika sekesheni za mita 2.45.
- KAMPUNI ina haki ya kuthibitisha utengenezaji wa mabomba ya HDPE yaliyowekwa katika kiwanda cha uzalishaji cha Mtengenezaji kulingana na mfumo wa usimamizi wa ubora kulingana na ISO 9001: 2015. Mfumo wa usimamizi wa ubora wa mtengenezaji utahitatakika kuwa uliothibitishwa kwa ISO 9001: 2015 na chombo cha uthibitisho cha Kimataifa.
- Malighafi inayotumika kutengeneza ukuta wa muundo wa bomba za HDPE na viunganishi vyake lazima vilingane na EN13476-1 / ISO 21138-1. Mahitaji ya ubora wa Bomba za HDPE na upimaji wao ni utahitajika kulingana na viwango EN13476-2 / ISO 21138-2, na marekebisho yake husika. Mahitaji ya ubora wa viunganishi zilizotengenezwa kutoka kwa muundo wa bomba za HDPE zitahitajika kulingana na EN 13476-2 / ISO 21138-2, na marekebisho yake ya hivi karibuni.
- Mabomba yote ya HDPE yaliyotengenezwa kwa ukuta yatakayotolewa dhidi ya Zabuni hii "yatatiwa alama" kulingana na viwango vya sahihi vinavyotumika.
- Kwa ombi, nyaraka za ubora wa bidhaa zinazotolewa zinapaswa kuwasilishwa na mtengenezaji kupitia vyeti vya kufanya kazi kulingana na viwango vinavyotumika. Rekodi zote za matokeo ya vipimo vya ubora zitahifadhiwa na mtengenezaji kwa marejeleo yajayo.
- Kabla na baada ya kutoa zabuni kwa Mtengenezaji, KAMPUNI ina haki ya kukagua uwezo wa upimaji na kushuhudia majaribio yaliyofanywa katika kituo cha Maabara cha Mtengenezaji kutathmini ubora wa bidhaa kulingana na viwango vinavyotumika. KAMPUNI itateua mwakilishi kushuhudia majaribio yote yaliyofanywa katika kituo cha maabara cha Mtengenezaji na mwakilishi atawasilisha matokeo yote ya mkandarasi/mzabuni husika & KAMPUNI kwa kujitegemea. KAMPUNI ina haki ya kuidhinisha Bidhaa kulingana na ripoti za majaribio ya ubora kabla ya kupelekwa kwenye eneo la ujenzi.

**VIGEZO MUHIMU VYA KUZINGATIA**

Taasisi zitakazoonesha nia zinaalikwa kuambatanisha maombi yao pamoja na taarifa zifuatazo:

- Uzoefu, utendaji, na uwezo katika kutekeleza kazi zilizoainishwa chini ya upeo wa kazi, kwa kiwango kikubwa nchini Tanzania, kwa kufuata viwango vya kitaifa na kimataifa (ikiwa ni pamoja na Viwango vya Shirika la Fedha la Kimataifa (IFC), na uzoefu wa angalau miaka 15 katika utendaji wa huduma kama hizo ndani ya Tanzania au Kimataifa.
- Uthibitisho wa usajili wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) pamoja na cheti cha uthibitisho wa kulipa kodi kwa mwaka wa fedha uliopita.
- Maelezo mafupi kuhusu uzoefu na uwezo wa:

  Utekelezaji wa programu za aina hiyo kwa viwango vya fedha vya kimataifa kwa ajili ya miradi mikubwa yo miundombinu nchini Tanzania.
- Kusimamia miradi mikubwa na wakandarasi washirika.
- Kufanya kazi kwa kushirikiana na serikali za mitaa na sekta binafsi.
- Wafanyakazi waliopendekezwa kufanya kazi kwenye Mradi huu na ujuzi na uzoefu wao katika kutekeleza programu za aina hii.
- Inashauriwa, mwonyesha nia atume maombi ya kusajiliwa na kanzi data ya EWURA (LSSP) kama mtoaji na msambazaji wa huduma ndani ya nchi wakati wa kuwasilisha ombi la kuonesha nia ya kutekeleza shughuli za progamu.

Mawanda haya yanaweza kugawanywa kimkoa au kiutalaam na KAMPUNI inaruhusu Wazabuni kuwasilisha pendekezo kwa ajili ya kipengele kimoja, kadhaa au vyote.

Taasisi zenye nia na ambazo zina uwezo na rasilimali za kutekeleza shughuli au kazi zilizoorodheshwa hapo juu zinapaswa kuwasilisha nia kwa lugha ya kiingereza pamoja na kuambatanisha nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe kwa **eacop-tz.eoi.1000001@totalenergies.com** (ukubwa wa barua pepe 20 Mb) saa au kabla ya saa **11 jioni** za Afrika Mashariki (EAT) tarehe **09 Novemba 2021.**Kichwa cha Habari cha Barua Pepe kiwe ni **0010007214.**

**Muhimu:** Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na taasisi zitakazoonyesha nia ili kutengeneza orodha ya taasisi za awali zenye vigezo vinavyotakiwa. Taasisi zitakazokidhi vigezo tu ndiyo zitapokea na kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA) pamoja na mwaliko wa kuwasilisha zabuni katika kuendeleza mchakato wa zabuni. Maelezo yote ya kuonyesha nia yanapaswa kuandikwa kwa lugha ya Kiingereza.

216553602

# BIASHARA YACHINJIWA BAHARINI MTOANO CAF

**Na Adam Fungamwango**

PAMOJA na kushinda mabao 2-0 kwenye mechi ya raundi ya kwanza ya Kombe la Shirikisho Afrika (CAF), ikishiriki kwa mara ya kwanza kwenye historia yake, timu ya Biashara United imetolewa katika michuano hiyo baada ya kushindwa kwenda kwenye mechi ya mkondo wa pili dhidi ya Al Ahli Tripoli, iliyopangwa kuchezwa Oktoba 23, Benghazi nchini Libya.

Taarifa iliyotolewa jana na Shirikisho la Soka Afrika (CAF) kupitia kwa Shirikisho la Soka nchini (TFF), imeeleza kuwa, uamuzi huo umefanywa na Kamati ya Mashindano ya CAF hivyo kuipa ushindi Al Ahli Tripoli kuendelea na michuano hiyo, ambapo sasa itacheza dhidi ya Stade Malien ya nchini Mali.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo ya TFF, kamati hiyo ya CAF, imeeleza sababu zilizoifanya Biashara United kushindwa kwenda nchini Libya kucheza mechi hiyo, hazikutokana na dharura.

Awali, Biashara United iliandika barua kutaka mechi hiyo isogezwe mbele kwa madai ya kushindwa kupata vibali vya kutumia anga za nchi za Sudan Kusini, Sudan na Libya, baada ya kupata ndege ya kukodi kutoka serikalini kwa kushirikiana na TFF.

Na hii ilikuja baada ya kuonekana timu hiyo imekwama kuondoka nchini kwa wakati kuwahi mechi hiyo.

Nipashe lilipomtafuta Ofisa Habari na Mawasiliano wa TFF, Cliford Ndimbo kujua endapo kuna adhabu kwa Biashara United iliyoambatana na kuondolewa huko, alisema kwa sasa walichokipokea ni kuondolewa tu.

"Ni taarifa hiyo tu ambayo kwa sasa tumeipokea, hakuna nyingine, labda kama itafuatа baadaye, hivyo kwa sasa tumebakiwa Simba pekee kwenye mashindano ya CAF, " alisema.

Tayari Yanga iliyokuwa ikiiwakilisha nchi kwenye Ligi ya Mabingwa na Azam FC Kombe la Shirikisho Afrika, zilishatupwa chini kwenye michuano hiyo inayoongoza kwa utajiri barani Afrika kwa ngazi ya klabu.

Biashara United katika mechi ya kwanza iliyochezwa nchini Oktoba 15, ilishinda mabao 2-0, kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, hivyo ilikuwa ikihitaji, ushindi ama sare ya aina yoyote au kutoruhusu kufungwa zaidi ya bao moja ili kusonga mbele.

## Taifa Jang'ombe yaipania Mlandege leo

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

BAADA ya kukubali sare katika mechi yao ya kwanza ya Ligi Kuu Zanzibar msimu huu dhidi ya Uhamiaji FC juzi, Kocha wa timu ya Taifa Jang'ombe, Omar Khamis 'Matu', amewaahidi mashabiki wa timu hiyo kuwa mchezo wa pili leo watahakikisha wanapata alama zote tatu.

Taifa Jang'ombe katika mchezo wake wa kwanza wa ligi hiyo dhidi ya Uhamiaji walitoka sare ya bila kufungana kwenye mchezo iliyopigwa Uwanja wa Amaan na kuhudhuria mashabiki wengi.

Leo Taifa Jang'ombe itavaana na Mlandege ambayo ina alama tatu baada ya mchezo wa kwanza kupata ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Machomane.

Kocha wa Taifa Jang'ombe, Matu akizungumza na mwandishi wetu jana, alisema lengo lao ni kupata ushindi katika mechi hiyo ya leo ili kuendeleza hamasa walioipata kutoka kwa mashabiki wao baada ya timu hiyo kupanda daraja msimu huu.

"Tumejipanga kupata alama tatu muhimu, mchezo wa kwanza tuseme tumepoteza kwa sare kwa kuwa tulikuwa na wachezaji majeruhi wa kikosi cha kwanza ambao hawakucheza, lakini sasa wamepona tutakuwa nao katika mchezo wa pili," alisema.

Aidha, alisema anaiheshimu timu ya Mlandege kwa kuwa ndio timu kongwe katika soka la Zanzibar, hivyo ili mipango yake itimie, lazima atumie mbinu ambazo zitamfanya kupata ushindi.

Taifa Jang'ombe itashuka dimba la Amaan leo kuvaana na Mlandege majira ya saa moja usiku wakati saa kumi jioni timu ya KMKM itavaana na Machomane, na katika Dimba la Mau majira ya saa nane mchana timu ya KVZ itakuwa na kibarua kigumu dhidi ya Maafande wenzao wa Mafunzo.

Katika Uwanja wa Gombani, Pemba siku hiyo, Polisi watavaana na Selem View majira ya saa kumi alasiri.

**BADO MBILI TU...**



Beki wa Kati wa Simba, Henock Inonga Baka 'Varane' (juu), akiwa mazoezini wakati huu akitumikia adhabu ya kadi nyekundu aliyoipata kwenye mechi ya Ligi Kuu dhidi ya Coastal Union Jumapili iliyopita katika Uwanja wa Benjamin Mkapa timu hizo zikitoka suluhu. Simba jana iliikaribisha Namungo FC uwanjani hapo, hivyo bado mechi mbili kabla ya beki huyo kurejea dimbani. Pembeni ni Mohamed Hussein 'Tshabalala'. **PICHA: SIMBA**

## Azam FC, Lwandamina sasa utamu kolea

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Azam FC imenogewa na uwezo wa Kocha wake Mkuu, Mzambia George Lwandamina baada ya kuamua kumwongeza mkataba wa mwaka mmoja wa kuendelea kusalia katika dimba la Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam.

Shughuli za utiaji saini mkataba huo zilifanyika Jumatatu wiki hii kwenye ukumbi maalum ndani ya Uwanja wa Azam Complex, chini ya Ofisa Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo, Abdulkarim Amin 'Popat'.

Kupitia mtandao rasmi wa Klabu ya Azam, imetoa picha kadhaa na maelezo mafupi kuhusiana na tukio hilo.

**"Kocha wetu Mkuu, George Lwandamina ameongeza mkataba wa mwaka mmoja, kuendelea kuwa nasi katika viunga vya Azam Complex, Chamazi. Shughuli ya utiaji wa saini wa nyongeza hiyo ya mkataba ilifanyika Jumatatu, Novemba Mosi kwenye ukumbi wa wageni maalum ndani ya Uwanja wa Azam Complex mbele ya Mtendaji Mkuu, Abdulkarim Amin 'Popat'.**

"Alijiunga nasi Novemba mwaka jana na hadi sasa ameiongoza timu yetu katika mechi 36 za mashindano yote," taarifa ilieleza.

Lwandamina, kocha wa zamani wa Yanga, ameiongoza Azam kwenye michezo 36, huku 25 ikiwa ni ya Ligi Kuu, minne ya Kombe la Shirikisho, mitano ya Kombe la Mapinduzi na mechi nne za Kombe la Shirikisho barani Afrika (CAF).

Juzi, aliiongoza Azam kushinda bao 1-0 dhidi ya Geita Gold na kuifanya timu hiyo kushika nafasi ya saba kabla ya mechi za jana, ikiwa na pointi saba kwa mechi tano, kwa kushinda mbili, sare moja na kupoteza mbili.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### KANE KUTOONDOKA SPURS
MSHAMBULIAJI wa England, Harry Kane mwenye umri wa miaka 28, ataachana na mipango ya kuondoka Tottenham Hotspur baada ya kuwasili kwa Antonio Conte kuifundisha klabu hiyo. **(Sun)**

### CONTE KWA DE VRIJ NAE
KOCHA mpya wa Tottenham Hotspur, Antonio Conte pia anaitaka Tottenham imsajili mlinzi wa Uholanzi na Inter Milan, Stefan de Vrij mwenye umri wa miaka 29 wakati wa dirisha la Januari. **(Football Insider)**

### POGBA ANAITAKA JUVENTUS
PAUL Pogba wa Manchester United anapendelea kurejea Juventus badala ya kujiunga na Paris St-Germain au Real Madrid wakati kiungo huyo wa kati wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 28, atakapokuwa mchezaji huru msimu ujao. **(Gazzetta dello Sport)**

### HAALAND KWENDA BARCELONA
ERLING Haaland amepanga kuondoka Borussia Dortmund na wakala wake anataka mshambuliaji huyo wa Norway mwenye umri wa miaka 21, ajiunge na Barcelona.**(El Nacional)**

### KASSIE AWANIWA TOTTENHAM
ANTONIO Conte anajiandaa kwa usajii wa kwanza wa kiungo wa kati wa AC Milan, Franck Kessie, akiwa kocha mpya wa Tottenham Hotspur. (Metro, via Sportitalia)

### HAZARD ATAJWA NEWCASTLE
MSHAMBULIAJI wa Real Madrid, Eden Hazard anaweza kujiunga na Newcastle United wakati wa dirisha la usajili la Januari, huku kocha Carlo Ancelotti akijiandaa kumwachia Mbelgiji huyo mwenye umri wa miaka 30. **(Star)**

### BROZOVIC ATAKIWA NEWCASTLE
NEWCASTLE United wanapanga uhamisho wa mchezaji wa Inter Milan, Marcelo Brozovic, huku kiungo huyo mkabaji wa Croatia mwenye umri wa miaka 28, akimaliza mkataba wake msimu ujao. **(Sun)**

### MARTINEZ NAFASI KUBWA
LICHA ya Unai Emery kuwa na nafasi kubwa ya kutua Newcastle, kocha wa Ubelgiji, Roberto Martinez anahimizwa kubeba mikoba ya ukocha kenye klabu hiyo. **(Football Insider)**

### JOHNSTONE ATAJWA WEST HAM
KLABU za Tottenham Hotspur, West Ham na Southampton zinamfukuzia mlinda mlango wa West Brom, Sam Johnstone mwenye umri wa miaka 28, ambaye mkataba wake unamalizika majira yajayo ya joto. **(Sky Sports)**

### VLAHOVIC LULU SPURS, JUVE
TOTTENHAM Hotspur ipo tayari kuchuana na Juventus kumnasa mshambuliaji wa Fiorentina, Mserbia Dusan Vlahovic mwenye umri wa miaka 21. **(Calciomercato)**

### ERIKSEN HUYOOO AJAX
NYOTA Christian Eriksen yuko tayari kujiunga tena na Ajax Januari, kwani kiungo huyo wa kati wa Denmark mwenye umri wa miaka 29, hawezi kuichezea klabu yake ya sasa ya Inter Milan akiwa amewekewa kifaa cha kudhibiti mapigo ya moyo. **(Corriere dello Sport)**

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# SOLSKJAER: RONALDO KAMA JORDAN WA CHICAGO BULLS

●●●Wakati mwingine timu inahitaji wachezaji wa namna hii na ndio maana amekuwa mtu muhimu zaidi kwetu...

**ROME, Italia**

OLE Gunnar Solskjaer amemlinganisha Cristiano Ronaldo na gwiji wa zamani wa mchezo wa mpira wa Kikapu wa Marekani, Michael Jordan baada ya mshambuliaji huyo kuipa Manchester United sare ya mabao 2-2 dhidi ya Atalanta kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya juzi, Jumanne.

Ronaldo alifunga mara mbili kwa United wakitoka nyuma na kusawazisha mabao ya Josep Ilicic na Duvan Zapata wakati 'Mashetani Wekundu' hao wakipata sare hiyo.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno, alifunga mabao hayo mawili ambayo yamefuta rekodi mbaya ya Man United ya kupoteza mechi nne mfululizo za ugenini kwenye michuano ya Ulaya kwa mara ya kwanza.

Pia imeifanya Man United kupaa kileleni mwa msimamo wa kundi lake wakilingana pointi na Villarreal, huku wakiwapita pointi mbili Atalanta.

Ronaldo pia amekuwa mchezaji wa pili mwenye umri mkubwa zaidi kufunga mabao mawili kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya baada ya Filippo Inzaghi (miaka 37 na siku 86), akifanya hivyo Novemba mwaka 2010.

Na Solskjaer ameelezea mchango wa mshambuliaji huyo na kulinganisha na nyota wa zamani wa timu ya Kikapu ya Chicago Bulls, Jordan.

"Wote tuna majukumu yetu," alisema Solskjaer akiwaambia waandishi wa habari baada ya mchezo huo.

"Cristiano ni kiongozi wa kundi, lakini kubwa analolifanya ni kufunga mabao.

"Hatuna furaha kuruhusu mabao mawili. Kwa hakika kabisa ni mchezaji muhimu kwetu. Ni kama vile Chicago Bulls walivyokuwa wanasaidiwa na Michael Jordan.

"Wakati mwingine timu inahitaji wachezaji wa namna hii na ndio maana amekuwa mtu muhimu zaidi kwetu."

MECHI KALI
HOME
AWAY
RACING GENK
3.49 | 3.54 | 2.04
WEST HAM

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#,
CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
halopesa
airtel money
EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

CHEZA USHINDE
JACKPOT TZS. 642

# EMERY AIKATAA NEWCASTLE UNITED



**MADRID, Hispania**

UNAI Emery atakataa nafasi ya kuwa kocha mpya wa Newcastle United na badala yake ataendelea kubaki Villarreal, kwa mujibu wa Guillem Balague.

Kocha huyo wa zamani wa Arsenal alithibitisha Jumanne kwamba amewasiliana na klabu hiyo ya Ligi Kuu, ambayo inataka kumfanya kuwa kocha wa kwanza kuchukua nafasi ya Steve Bruce.

Vyanzo vilivyopo karibu na Emery mwenye umri wa miaka 50, vimedai kuwa kocha huyo anaona kwamba wamiliki wapya wa klabu hiyo 'Magpies' hawana dira nzuri.


Newcastle ilikuwa na matumaini ya kumpata raia huyo wa Hispania wikendi iliyopita.

Lakini mchambuzi wa soka la Hispania, Balague amesema wale wote wanaomshauri Emery hawana uhakika na mipango ya klabu hiyo.

"Emery alikuwa na presha kubwa (kwenye mchezo wao wa ushindi wa 2-0 wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Young Boys, Jumanne)," alisema Balague.

"Na kunaonekana wazi kwamba, klabu haina dira nzuri na yeye hana mpango wa kwenda huko."

# Lewandowski bora zaidi duniani – Nagelsmann



**MUNICH, Ujerumani**

KOCHA Mkuu wa Bayern Munich, Julian Nagelsmann, amepaza sauti na kusema Robert Lewandowski ataendelea kuwa mshambuliaji bora zaidi duniani wakati mchezaji huyo akifunga mabao matatu 'hat-trick' kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya wakiibuka na ushindi wa mabao 5-2 dhidi Benfica juzi, Jumanne.

Lewandowski alifikisha mechi 100 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya wakati Bayern ikiifunga Benfica mabao 5-2 na kutangulia kwenye hatua ya 16-bora kutoka Kundi E.

Nyota huyo ambaye yupo kwenye kinyang'anyiro cha kuwania tuzo ya Ballon d'Or, amekuwa mchezaji wa sita kufunga katika mechi yake ya 100 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, baada ya Thierry Henry, Zlatan Ibrahimovic, Cristiano Ronaldo, Andrea Pirlo na Toni Kroos.

Hata hivyo, nahodha huyo wa timu ya Taifa ya Poland amekuwa mchezaji wa kwanza kufunga zaidi ya bao moja kwenye mchezo wa 100 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Lewandowski pia hiyo ilikuwa hat-trick yake ya nne kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya na kuwa mchezaji wa tatu mwenye hat-trick nyingi nyuma ya Ronaldo na Lionel Messi (wote wana nane).

Katika umti wa miaka 33 na siku 73, ni mchezaji wa nne mwenye umri mkubwa zaidi kufunga hat-trick kwenye michuano hiyo baada ya Olivier Giroud (miaka 34 na siku 63), Ronaldo na Claudio Pizarro (miaka 34 na siku 35).

Nagelsmann alimsifia Lewandowski baada ya mchezo huyo akiwaambia waandishi wa habari: "Amehusika katika mabao 81 kwenye mechi 100 za Ligi ya Mabingwa Ulaya. Kitu kipya?

Wakati alipoulizwa kumlinganisha Lewandowski na akina Ronaldo na Messi, Nagelsmann alisema: "Nafikiri ni ngumu sana kuwalinganisha kwa sababu ni wachezaji ambao ni tofauti kabisa.

"Lakini naamini ataendelea kufunga na kuwa mshambuliaji namba moja duniani, hilo halina ubishi kabisa."

## HABARI MICHEZO


2,668,240

JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 06/11/21 | 18:00 | Crystal Palace vs Wolverhampton | 2.42 | 3.14 | 3.04 |
| 02. 06/11/21 | 18:00 | Blackburn vs Sheffield Utd | 2.32 | 3.29 | 2.89 |
| 03. 06/11/21 | 18:00 | Luton Town vs Stoke City | 2.27 | 3.21 | 3.06 |
| 04. 06/11/21 | 18:00 | Barnsley vs Hull City | 2.44 | 3.09 | 2.89 |
| 05. 06/11/21 | 20:30 | Alaves vs Levante | 2.55 | 3.05 | 2.95 |
| 06. 06/11/21 | 20:30 | Blackpool vs QPR | 2.44 | 3.28 | 2.74 |
| 07. 07/11/21 | 17:00 | Everton vs Tottenham | 2.65 | 3.15 | 2.75 |
| 08. 07/11/21 | 17:00 | Nantes vs Strasbourg | 2.38 | 3.23 | 2.98 |
| 09. 07/11/21 | 17:00 | Leeds vs Leicester | 2.85 | 3.45 | 2.39 |
| 10. 07/11/21 | 17:00 | Udinese vs Sassuolo | 2.47 | 3.44 | 2.75 |
| 11. 07/11/21 | 20:30 | Osasuna vs Real Sociedad | 2.94 | 3.24 | 2.43 |
| 12. 07/11/21 | 22:45 | Rennes vs Lyon | 2.89 | 3.48 | 2.32 |
| 13. 07/11/21 | 23:00 | Betis vs Sevilla FC | 2.80 | 3.21 | 2.55 |

MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

ALHAMISI - 04 - NOVEMBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 1758 | Khimki M-SKA vs Khabarovsk-M | 2.80 | 3.65 | 2.34 |
| 14:00 | 1262 | Otmk Olmaliq vs FC Andijon | 1.23 | 5.40 | 9.63 |
| 15:00 | 4192 | Bkma Yerevan vs Van Yerevan | 3.67 | 3.14 | 1.96 |
| 15:00 | 5600 | FC Kairat Moscow vs FC Chita | 1.74 | 3.95 | 4.30 |
| 16:00 | 1439 | Misr Lel Makasa vs Ceramica Cleopatra | 3.65 | 3.21 | 2.04 |
| 16:00 | 5122 | National Bank vs Ismaily SC | 2.57 | 3.07 | 2.77 |
| 16:30 | 2117 | AS Slimane vs US Monastir | 3.07 | 2.81 | 2.39 |
| 16:30 | 4721 | ES Sahel vs Sportive Zarzis | 1.35 | 4.30 | 7.80 |
| 17:15 | 3880 | Al Khoor vs Al Arabi Doha SC | 3.96 | 3.96 | 1.68 |
| 17:15 | 5889 | Qatar SC vs Al-Sailiya SC | 1.74 | 3.73 | 3.87 |
| 18:30 | 2241 | Arab Contractors vs Talaea El Gaish | 2.71 | 3.10 | 2.61 |
| 18:30 | 4209 | Flora Tallinn vs Anorthosis Famagusta | 2.41 | 3.40 | 2.85 |
| 18:30 | 5300 | Kairat Almaty vs Karabakh | 2.80 | 3.31 | 2.49 |
| 18:30 | 5666 | Africain vs Olympique de Beja | 1.78 | 2.89 | 5.21 |
| 20:45 | 1200 | Real Sociedad vs Sturm Graz | 1.21 | 6.40 | 13.00 |
| 20:45 | 1744 | Maccabi Tel Aviv vs HJK Helsinki | 1.33 | 5.20 | 8.60 |
| 20:45 | 2000 | Brondby vs Rangers | 3.76 | 3.61 | 1.93 |
| 20:45 | 2147 | AZ Alkmaar vs CFR Cluj | 1.36 | 4.89 | 8.39 |
| 20:45 | 2624 | Olympiakos vs Eintracht Frankfurt | 2.43 | 3.44 | 2.79 |
| 20:45 | 2844 | Zorya Lugansk vs CSKA Sofia | 2.13 | 3.41 | 3.36 |
| 20:45 | 2989 | LASK Linz vs Alashkert Martuni | 1.17 | 7.38 | 14.95 |
| 20:45 | 3646 | Monaco vs PSV Eindhoven | 2.19 | 3.56 | 3.11 |
| 20:45 | 4010 | Lyon vs Sparta Prague | 1.42 | 4.90 | 6.60 |
| 20:45 | 4201 | Racing Genk vs West Ham | 3.49 | 3.54 | 2.04 |
| 20:45 | 4917 | Legia Warszawa vs Napoli | 7.19 | 4.99 | 1.39 |
| 20:45 | 4968 | Galatasaray vs Lokomotiv Moscow | 1.72 | 3.84 | 4.59 |
| 20:45 | 5396 | Randers vs Baumit Jablonec | 1.98 | 3.60 | 3.60 |
| 20:45 | 5613 | Omonia Nicosia vs FC Basel | 3.25 | 3.70 | 2.08 |
| 20:45 | 5679 | Lincoln FC vs Slovan Bratislava | 6.60 | 4.26 | 1.48 |
| 20:45 | 5706 | KAA Gent vs Partizan | 1.97 | 3.55 | 3.70 |
| 21:00 | 3948 | Burgos vs Zaragoza | 2.70 | 2.95 | 2.70 |
| 21:00 | 5130 | Girona vs Alcorcon | 1.58 | 3.67 | 5.67 |
| 21:30 | 3796 | Farul Constanta vs Steaua Bucuresti | 2.51 | 3.15 | 2.75 |
| 22:45 | 2012 | Drogheda Utd vs Dundalk FC | 3.37 | 3.32 | 1.99 |
| 23:00 | 1036 | Rennes vs NK Mura | 1.14 | 7.81 | 18.02 |
| 23:00 | 1168 | Dinamo Zagreb vs Rapid Vienna | 1.77 | 3.81 | 4.32 |
| 23:00 | 1608 | PAOK vs Copenhagen | 2.22 | 3.41 | 3.16 |
| 23:00 | 2134 | Roma vs Bodo Glimt | 1.35 | 5.39 | 7.58 |
| 23:00 | 2135 | Marseille vs Lazio | 2.28 | 3.41 | 3.06 |
| 23:00 | 2649 | Red Star Belgrade vs Midtjylland | 1.90 | 3.59 | 3.94 |
| 23:00 | 2790 | Bayer Leverkusen vs Betis | 2.00 | 3.65 | 3.50 |
| 23:00 | 3165 | Ferencvaros TC vs Celtic | 3.18 | 3.38 | 2.22 |
| 23:00 | 3783 | Union Berlin vs Feyenoord | 2.24 | 3.50 | 3.05 |
| 23:00 | 3814 | Royal Antwerp vs Fenerbahce | 2.64 | 3.29 | 2.64 |
| 23:00 | 3819 | Sporting Braga vs Ludogorets Razgrad | 1.41 | 4.70 | 7.21 |
| 23:00 | 3864 | Slavia Prague vs Maccabi Haifa | 1.52 | 4.19 | 6.18 |
| 23:00 | 3870 | Leicester vs Spartak Moscow | 1.33 | 5.42 | 8.24 |
| 23:00 | 5413 | Tottenham vs Vitesse Arnhem | 1.30 | 5.40 | 9.41 |
| 23:15 | 2960 | Malaga vs Real Sociedad B | 1.69 | 3.43 | 5.10 |
| 23:15 | 4798 | UD Ibiza Eivissa vs Tenerife | 2.39 | 3.00 | 3.05 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# KOCHA BARCELONA ASUBIRIA MIUJIZA



**KIEV, Ukraine**

SERGI Barjuan hafikirii kuhusu majaliwa yake kama kocha wa muda wa Barcelona baada ya ushindi wa bao 1-0 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Dynamo Kiev, Jumanne.

Lakini amesema Mungu ataamua kama ataendelea kuwa katika nafasi hiyo baada ya mchezo wa Jumamosi inayokuja dhidi ya Celta Vigo kwenye Ligi Kuu Hispania, LaLiga.

Barca iliongeza matumaini yao ya kufuzu hatua ya 16-bora baada ya kupata ushindi wa pili mfululizo kwenye michuano hiyo kwa kuifunga Dynamo, licha ya kwamba hawakuonyesha kiwango cha kuvutia pale mjini Kiev.

Bao la Ansu Fati la kipindi cha pili liliisaidia Barca kujivuta hadi nafasi ya pili kwenye Kundi lao la E, wakati huu kukiwa na uvumi wa ujio wa Xavi kuchukua mikoba ya ukocha ya Ronald Koeman aliyetimuliwa.

Barca itasafiri kuifuata Celta mwishoni mwa wiki hii, huku Sergi akiwa hana uhakika kama ataendelea kuwa kocha wa kikosi hicho au atarudi kuinoa Barcelona B.

"Niliwaambia wao (wachezaji) namna gani mchezo ulikuwa muhimu kabla ya mchezo huo," alisema Sergi.

"Jambo la msingi ni kwamba tumeshinda, lakini sijui nini kinachofuata kwa sasa.

"Leo (juzi) tumeshinda na kufurahi. Tunafurahia kwa muda. Mungu ataamua kama tutamaliza wiki vizuri dhidi ya Vigo."

# Tuchel ataka zaidi kutoka kwa Ziyech

**STOCKHOLM, Sweden**



THOMAS Tuchel anataka kuona kuimarika zaidi kwa Hakim Ziyech licha ya raia huyo wa Morocco kuifungia Chelsea wakati ikiibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Malmo, Jumanne.

Chesea wakiwa wameanza vibaya kipindi cha kwanza kwenye mchezo huo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya pale kwenye dimba la Eleda, walipata bao hilo dakika ya 11 baada ya kuanza kipindi cha pili likifungwa na Ziyech.

Hilo lilikuwa bao lake la kwanza kwa Ziyech tangu alipofungwa kwenye UEFA Super dhidi ya Villarreal, Agosti na la tatu kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya katika mechi 13 alizowachezea 'Blues' hao.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, alionekana kuwa kwenye kiwango bora zaidi katika mchezo huo uliopigwa nchini Sweden akifunga kwa kuunganisha pasi ya Hudson-Odoi.

Na Tuchel, ambaye alimsifia nyota huyo baada ya mchezo huo, alisema anataka kuona mengi zaidi kutoka kwa Ziyech. "Alikuwa na mchezo mzuri na kwa hakika nampongeza kwa hilo," alisema Tuchel.

"Bado naona kuna nafasi kwake yeye kuendelea kuimarika zaidi. Anaweza kuwa bora zaidi ya alivyo sasa.

"Bado hajawa fiti kwa asilimia 100 kama ambavyo anatakiwa kuwa, lakini ninaamini ataimarika zaidi."

Michezo

Alhamisi Novemba 4, 2021

Nipashe



## Solskjaer: Ronaldo kamaJordan wa Chicago Bulls

UKURASA 21


SOMA HIYOOO!...



Kiungo wa Yanga, Feisal Salum 'Fei Toto' (mbele), akishangilia sambamba na beki wa timu hiyo Djuma Shabani, baada ya kuifungia timu yake bao la kusawazisha wakati wakishinda 3-1dhidi ya Ruvu Shooting kwenye mechi ya Ligi Kuu iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Biashara yachinjiwa baharini mtoano CAF

**Na Adam Fungamwango**




PAMOJA na kushinda mabao 2-0 kwenye mechi ya raundi ya kwanza ya Kombe la Shirikisho Afrika (CAF), ikishiriki kwa mara ya kwanza kwenye historia yake, timu ya Biashara United imetolewa katika michuano hiyo baada ya kushindwa kwenda kwenye mechi ya mkondo wa pili dhidi ya Al Ahli Tripoli, iliyopangwa

UK. 20

## Lewandowski atajwa bora zaidi duniani



**MUNICH, Ujerumani**

KOCHA Mkuu wa Bayern Munich, Julian Nagelsmann amepaza sauti na kusema Robert Lewandowski ataendelea kuwa mshambuliaji bora zaidi duniani wakati mchezaji huyo akifunga mabao matatu 'hat-trick' kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya wakiibuka na ushindi wa mabao 5-2 dhidi Benfica juzi, Jumanne.

UK. 22

# MKWASA: NYOTA WA MECHI YANGA NI REFA

●●●Alia kukandamizwa akiitaja penalti isiyostahili huku akisema kama si Mwandembwa kuibeba...

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kushuhudia Yanga ikitokea nyuma kwa bao 1-0 na kushinda 3-1 kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa juzi katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Kocha Mkuu wa Ruvu Shooting, Boniface Mkwasa, ameulalamikia uchezeshaji wa mwamuzi Emmanuel Mwandembwa wa Arusha, kuwa chanzo cha kipigo hicho kutokana na maamuzi yake ya kuwakandamiza.

Akizungumza baada ya mechi hiyo ya Ligi Kuu Tanzania Bara, Mkwasa alisema kuwa kila mwenye macho ameona na mwamuzi huyo ndiye aliyekuwa nyota wa mchezo huo ('Man of the Match' ) kwa kufanya matukio kadhaa ya kuwatoa wachezaji wake mchezoni.

"Kila mtu aliona kilichotokea, kwa sababu tuliingia na mpango mkakati ambao ulikuwa umekaa vizuri, lakini mwamuzi aliamua kututoa kwenye mchezo, naheshimu maamuzi, lakini kwenye mechi hii 'Man of the Match' (Nyota wa Mchezo) alikuwa mwamuzi kwa kuwatoa wachezaji wangu kwenye morali," alisema kocha huyo wa zamani wa Yanga.

Matukio ambayo Ruvu Shooting wamekuwa wakilalamikia ni kutolewa kwa kadi nyekundu beki wao, Santos Mazengo, pamoja na penalti ambayo picha za marudio zinaonyesha kuwa mpira huo ulishikwa na mshambuliaji wa Yanga, Fiston Mayele na mwamuzi aliamuru 'tuta', huku akimwonya kwa kadi ya njano beki Ally Mtoni 'Sonso' kwa madai kuwa ndiye aliyeunawa.

Hata hivyo, Mkwasa alisema kuwa timu yake haikucheza vibaya, ni kwa sababu tu walikuwa pungufu kwa mchezaji mmoja kwa muda mrefu.

"Yanga walikuwa na faida ya kuwa na mtu mmoja zaidi, na kwa sababu wana uwezo wa kukaa na mpira na sisi muda mrefu tunaufutafuta, ilisababisha wachezaji wangu kuchoka," alisema.

Naye Makamu Mwenyekiti wa Yanga, Fredrick Mwakalebela, alisema kikosi chao kinaonyesha kuwa kinaendelea kubadilika kila kukicha, kwani pamoja na kutanguliwa bao, lakini hawakuhamaki.

"Wachezaji walitulia na kuweza kurudisha goli na kupata mengine ya ushindi," alisema Mwalalebela ambaye amekiri ugumu wa Ligi Kuu msimu huu.

"Ni msimu mgumu kwa sababu timu nyingi zimeleta wachezaji vijana wenye uwezo mkubwa wa kupambana, tumeona matokeo mengine ya kikatili kama wenzetu wanapambana sana, lakini mwisho wa siku hawapati matokeo na hii ni kulishukuru Shirikisho la Soka nchini (TFF) kwa kuifanya ligi kuwa bora kutokana na udhamini," alisema Mwakalebela.

Yanga imefikisha pointi 15, ikiwa kileleni, Ruvu Shooting ikiwa na pointi sita kwa timu hizo kila moja kushuka dimbani mara tano.

Kwa sasa ligi hiyo inaelekea mapumziko kupisha Kalenda ya Fifa ya mechi za kuwania kufuzu Kombe la Dunia mwakani nchini Qatar, ambapo kwa timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars itaikaribisha DR Congo Alhamisi ijayo katika Uwanja wa Benjamin Mkapa kabla ya Jumapili ya Novemba 14, mwaka huu kushuka dimbani nchini Madagascar kuwavaa wenyeji hao.

Ligi hiyo itarejea tena Novemba 19, kwa Ruvu Shooting kuikaribisha Simba wakati kesho yake Yanga wakiwa wageni wa Namungo FC walioshuka Uwanja wa Mkapa jana dhidi ya 'Wekundu wa Msimbazi'.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >